# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*




| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00059 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Aprili 10 - 16, 2024 |

## MSD yatoa msaada Rufiji

Uk. 2



## Benki Kuu yafafanua ongezeko la riba

Uk. 5



## Fenesi ni tiba ya saratani na moyo

Uk. 14



### VITA DHIDI YA MALARIA:

# Rais Samia azidi kuungwa mkono

- **Wadau wa Mfuko wa Afya wamwaga bil. 37.7/-**




# Wanajeshi watatu wa Tanzania Kikosi cha SADC wauawa DRC

**Na Mwandishi Wetu**

ASKARI watatu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kikosi cha SADC kilichopelekwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuisaidiana na askari wa nchi hiyo kupambana na waasi wa M23, wameuawa katika shambulio la kombora.

Taarifa zilizoripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari vya nje vikiwanukuu maafisa wa Kikosi cha SADC, vilieleza kuwa askari hao waliuawa wakiwa eneo la Mashariki mwa DRC.

Kikosi hicho cha SADC, kilipeleka wanajeshi katika Jimbo la Kivu Kaskazini Desemba, mwaka jana kusaidia Serikali ya Kinshasa kudhibiti tena maeneo yaliyotekwa na waasi wa M23 Mashariki mwa DRC.

Uk. 4



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alipokutana na Balozi wa Uswizi

# MSD `yawapiga jeki' waathirika mafuriko Rufiji

**Na Mwandishi Wetu**

BOHARI ya Dawa (MSD), imetoa bidhaa za afya mbalimbali kwa waathrika wa mafuriko katika Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani.

Meneja wa MSD Kanda ya Dar es Salaam, Betia Kaema, alisema MSD baada ya kuona taarifa ya janga la mafuriko, iliamua kuchukua hatua za haraka kuwasiliana na Mamlaka za Wilaya ili kufahamu mahitaji yanayotakiwa kwa waathirika.

"Leo (jana), tumekabidhi vifaa ili kuhakikisha huduma za afya hazisimami kwa wananchi, lakini pia tumetembelea maeneo mbalimbali kujionea athari za mafuriko haya. MSD itaendelea kutoa ushirikiano mpaka pale hali itakapotengamaa," alisema.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa bidhaa hizo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Dk. Hamis Abdallah, aliishukuru MSD kwa hatua za haraka zilizochukuliwa kuwasaidia waathirika hao.

Alisema bidhaa hizo zitasaidia katika utoaji wa huduma kwa waathirika wa mafuriko.

Bidhaa hizo zilikabidhiwa Kituo cha Afya Mohoro kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ambazo ni pamoja na dawa za kuzuia na kutibu malaria, dawa za kutibu kuharisha na magonjwa mengine ya milipuko kama vile kipindupindu.

Kwa upande wa vifaa ni pamoja na magodoro, mashuka na vyandarua, milingoti ya kutundikia maji tiba, binliners na vifaa vingine vitakavyosaidia katika zoezi hilo.



# Wahamiaji haramu 16 watiwa mbaroni Iringa

**Na Mwandishi Wetu**

WAHAMIAJI haramu 16 raia wa Ethiopia, wametiwaa mbaroni mkoani Iringa kwa tuhuma za kuingia nchini bila kibali.

Wahamiaji hao haramu, walikamatwa na Askari wa Uhamiaji kwa kushirikiana na polisi mkoani Iringa.

Akizungumza na vyombo vya habari mjini Mafinga juzi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alisema wahamiaji hao walikamatwa katika eneo la msitu wa Luganga Kata ya Sao Hill, wilayani Mufindi.

Alifafanua kuwa walikutwa wakiwa wametelekezwa katika shamba la mahindi baada ya kushushwa kwenye gari ambalo awali lilikuwa likisomeka namba za usajili STL 3999 aina ya Land Cruiser V8 lenye rangi nyeupe ambapo dereva wake aliliteleleza baada ya kuona anafuatiliwa na askari.

"Baada ya dereva huyo kuona anafuatiliwa na askari, akaona hataweza kupita barabara kuu, hivyo alipita njia nyingine na kufika sehemu ambako alikutana na tikiti (swap), hali iliyowafanya washindwe kuendelea na safari hiyo, ndipo alipowashusha wahamiaji hao na kuifunga na kutokomea kusikojulikana," alisema Kamanda Bukumbi.

**Baada ya dereva huyo kuona anafuatiliwa na askari, akaona hataweza kupita barabara kuu, hivyo alipita njia nyingine na kufika sehemu ambako alikutana na tikiti (swap), hali iliyowafanya washindwe kuendelea na safari hiyo, ndipo alipowashusha wahamiaji hao na kuifunga na kutokomea kusikojulikana."**

Alisema uchunguzi wa awali umebaini kwamba gari hilo limesajiliwa kwa namba T 803 CVW linalomilikiwa na mkazi mmoja wa Tabata jijini Dar es Salaam huku akieleza jitihada mbalimbali ambazo zinaendelea za kumtafuta dereva pamoja na mmiliki wa gari hilo.

Kwa upande wake, Afisa Uhamiaji wa Mkoa wa Iringa, Peter Kimario, alisema biashara hiyo haramu ya binadamu, ni mbaya kwani inahatarisha usalama wa Taifa.

"Kupitia vyombo vya habari, natoa wito kwa Watanzania watusaidie katika kampeni yetu ambayo imeanzishwa nchini mzima inayoitwa 'Mjue Jirani Yako' kwa sababu hawa tumewakamta kwenye magari ya aina hiyo, hivyo tunaamini wanaweza kutumia mbinu za kuvaa vizuri kama Watanzania na kusafiri katika vyombo vya usafiri vya kawaida bila kuwajua," alisema.

Alisema kampeni hiyo ya Mjue Jirani Yako, imeanzishwa ili kujua vitu ambavyo vinaendelea katika maisha ya wananchi kwa sababu usalama wa nchi, kila mtu anahusika katika jambo hilo.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa Jeshi la Uhamiaji litaendelea kushirikiana na vyombo vingine ili kuhakikisha wahamiaji hao wanafikishwa kwenye vyombo husika na kuchukuliwa hatua.

## Vigogo sita AICC wasimamishwa kazi

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

VIGOGO sita wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma za kukiuka taratibu na kanuni za uendeshaji wa mashirika ya umma.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano AICC, Freddy Maro, vigogo hao walisimamishwa kuanzia Aprili 3, mwaka huu.

Aliwataja kuwa ni Mkurugenzi wa Fedha na Utawala CPA Savo Mung'ong'o, Mkurugenzi wa Miliki na Miradi, Mhandisi Victor Kamagenge na Mkurugenzi wa Masoko na Mikutano, Mkunde Mushi.

Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu na Utawala, Festo Mramba, Mhasibu Mkuu CPA Augustine Karadoga na Meneja JNICC, Catherine Kilinda.

**Mkurugenzi wa Fedha na Utawala CPA Savo Mung'ong'o, Mkurugenzi wa Miliki na Miradi, Mhandisi Victor Kamagenge na Mkurugenzi wa Masoko na Mikutano, Mkunde Mushi.**


UMG
HII SI YA KUKOSA!
TAMASHA KUBWA
MITATU YA KISHINDO KAZI INAONGEA
APR 20th
SAA 1: 00 ASUBUHI
VIWANJA VYA TTCL KIJITONYAMA
#MIAKA MITATU YA KISHINDO
#KAZI INAONGEA
#MAMA YUKO KAZINI
TTCL
PSSSF
Public Service Social Security Fund
WCF
Workers Compensation Fund

## VITA DHIDI YA MALARIA:

# Rais Samia azidi kuungwa mkono

## • Wadau wa Afya wamwaga bil. 37.7/-

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WADAU wa Mfuko wa Afya, wameichangia Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Sh. bilioni 37.7 kusaidia kutokomeza malaria nchini, ifikapo mwaka 2030.

Wadau hao ni Uswisi, Denmark, Ireland, Korea Kusini, mashirika ya UNFPA, UNICEF na Benki ya Dunia, kupitia awamu ya ufadhili wa moja kwa moja wa Kituo cha Afya (DHFF) (2021-2025).

Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, alisema hayo wakati wa kikao na Balozi wa Uswisi nchini Didier Chassot, kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Afya jijini Dodoma juzi.

Alisema wizara yake kwa pamoja na wadau hao, wamejadiliana masuala yenye manufaa kwa pande zote mbili katika ushirikiano unaoendelea.

"Kwa niaba ya Serikali chini ya Rais Dk. Samia, tunashukuru kupitia kwako Balozi kwa msaada wa Serikali ya Uswisi na ahadi zako ambazo umezitoa katika kusaidia Sekta ya Afya kupitia michango mbalimbali ya ruzuku," alisema.

Alisema lengo la jumla la mradi ni kuchangia kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030 kupitia ushirikishwaji wa wadau wa kitaifa, baina ya kisekta na kikanda kwa kushawishi mijadala ya sera za kimataifa na miongozo ya kiufundi kwa kushirikishana desturi za Kitanzania.

"Mradi huu unawanufaisha Watanzania (Bara na Zanzibar) wanaokabiliwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa malaria hasa wale wa vijijini na wale walio katika makundi hatarishi zaidi (wajawazito na watoto, watu binafsi wanaoishi katika mazingira hatarishi)," alisema.

Aliiomba Serikali ya Uswizi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kutokomeza magonjwa ya ngono ikiwa ni pamoja na VVU, mimba zisizotarajiwa, ndoa za utotoni, ukatili wa kijinsia pamoja na kusaidia wahudumu wa afya ngazi ya jamii (CHWs) ambao wana jukumu katika kutoa huduma muhimu za afya kwa jamii.

Kwa upande wake, Balozi wa Uswisi nchini Chassot, alisema Serikali ya Uswisi itaendelea na dhamira yake ya kuisaidia Sekta ya Afya nchini ili kudumisha umoja uliopo baina ya nchi hizo mbili.

"Serikali ya Uswisi itachangia kwa pamoja na Serikali ya Ujerumani kwa lengo la kuendeleza umoja wetu kwa kutoa msaada wa kiufundi kwa njia ya kujenga uwezo kwa taasisi zilizopewa mamlaka na uidhinishaji wa Bima ya Afya kwa Wote (UHI)," alisema Balozi Chassot.



Waziri wa Afya Ummy Mwalimu

# Wanajeshi watatu wa Tanzania Kikosi cha SADC wauawa DRC

**Na Mwandishi Wetu**

ASKARI watatu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kikosi cha SADC kilichopelekwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuisaidiana na askari wa nchi hiyo kupambana na waasi wa M23, wameuawa katika shambulio la kombora.

Taarifa zilizoripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari vya nje vikiwanukuu maafisa wa Kikosi cha SADC, vilieleza kuwa askari hao waliuawa wakiwa eneo la Mashariki mwa DRC.

Kikosi hicho cha SADC, kilipeleka wanajeshi katika Jimbo la Kivu Kaskazini Desemba, mwaka jana kusaidia Serikali ya Kinshasa kudhibiti tena maeneo yaliyotekwa na waasi wa M23 Mashariki mwa DRC.

Kikosi hicho kinajumuisha wanajeshi wa Afrika Kusini, Tanzania na Malawi.

"Tukio hili la kusikitisha lilitokea baada ya kombora la adui kuanguka karibu na kambi ya wanajeshi hao," taarifa ya Kikosi cha SADC ilifafanua bila kutoa maelezo zaidi.

Juhudi za gazeti hili kumpata Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Stergomena Tax, kwa ufafanuzi zaidi kuhusiana na tukio hilo, hazikufanikiwa kwani simu yake ya mkononi iliita bila kupokelewa na hata alipotumiwa ujumbe kupitia simu yake, hakuujibu.

Hali kadhalika, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, simu yake iliita bila kupokelewa.



# 30 mbaroni tuhuma kughushi nyaraka za mafao

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na maofisa wa

Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), linawashikilia watu 30 kwa tuhuma za kughushi nyaraka zinazohusiana na mafao.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na maofisa, wamewakamata watu hao na kwamba hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa dhidi yao.

Alisema jeshi hilo linaendelea kusimamia mifumo mbalimbali ya kiuhalifu Dar es Salaam.

Kamanda Muliro alisema hatua za kisheria zikikamilika watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma hizo.

Aidha, Kamanda Muliro akizungumzia kuhusu mafanikio ya mfumo wa haki jinai, alisema kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu, watuhumiwa mbalimbali walipatikana na hatia wakiwamo wenye makosa ya kulawiti, kubaka na utapeli.

Alisema waliopatikana na hatia ya makosa ya kuingiliwa kinyume cha maumbile, kubaka na kulawiti, walihukumiwa adhabu za kifungo cha maisha, miaka 60 na 50 jela.

# BoT yafafanua ongezeko la riba

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema ongezeko la asilimia sita ya riba Benki Kuu limeongezwa ili kudhibiti mfumuko wa bei siku za usoni.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi BoT, Dk. Suleiman Missango, alisema mwenendo wa uchumi wa dunia, ulikuwa unaashiria uwepo wa mfumuko wa bei.

Alisema kutokana na hali hiyo, BoT ikaona iongeze riba kutoka asilimia 5.5 hadi asilimia sita katika robo ya pili kuanzia Aprili, mwaka huu.


Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi BoT, Dk. Suleiman Missango

Alisema kupanda kwa riba hiyo kumezingatia ukuaji wa uchumi kwa maana ya uwepo wa fedha za kutosha katika mzunguko kulingana na malengo yaliyowekwa.

"Wengi walijua tunakwenda kuweka ukomo wa riba, siyo kweli, kwa kupandisha riba hiyo maana yake tunapunguza ukwasi katika mzunguko na hivyo kudhibiti mfumuko wa bei kwa siku zijazo.

"Kupanda kwa riba hiyo, kumezingatia ukuaji wa uchumi, maamuzi mengine yatachukuliwa Julai mwanzoni na riba hii ni ya robo ya kwanza ya Aprili, mwaka huu na inaweza kupungua au kuongezeka kwa kadiri ya uchambuzi utakavyokuwa," alifafanua.

Pia alisema BoT imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na mabenki ili kudhibiti ujazi wa fedha katika mabenki na kwenye mzunguko.

"Tangu BoT ianzishe mfumo wa riba ya benki mwaka huu badala ya mfumo wa zamani wa ujazi wa fedha hali imeendelea kuwa tulivu na mapokeo yamekuwa mazuri kwa wadau," alisema.

Alisema hali hiyo imetokana na juhudi kubwa ya kutoa elimu kwa wadau katika sekta na imeahidi kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuweza kufanya uamuzi sahihi katika shughuli za kiuchumi.




## RC ataka weledi, huduma bora sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewataka watumishi wa sekta ya afya mkoani hapa, kuzingatia weledi na kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuakisi maboresho na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika sekta ya afya.

Amesema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya maboresho na ujenzi wa miundombinu ya afya kama vile majengo, ununuzi wa bidhaa za afya na kuwezesha ajira za kutosha, lengo likiwa kuinua hadhi ya huduma zinazotolewa nchini, hasa zinazowagusa wananchi wa kawaida.

Alitoa rai hiyo wakati wa akifungua kikao kazi baina ya Bohari ya Dawa (MSD) Kanda ya Iringa na wadau wake kutoka halmashauri saba za mkoani Ruvuma (Madaba Tc, Madaba Dc, Songea MC, Songea DC, Nyasa DC, Mbinga TC na Mbinga DC), kilichofanyika mjini Songea juzi.

Aliwakumbusha viongozi hao wa sekta ya afya mkoani hapa, kufanya maoteo yao ya bidhaa za afya kwa usahihi, umakini na kwa wakati ili kuiwezesha MSD kutekeleza majukumu yake ya ugavi wa bidhaa za afya kwa weledi.

Aliwataka pia watendaji hao kusimamia ukusanyaji wa mapato na kutumia vyema vyanzo vyao vingine vya mapato kulipa madeni ya MSD, huku akiwakumbusha pia kuhakiki taarifa sahihi za utunzaji na utoaji wa bidhaa za afya ili kuepuka upotevu wa bidhaa hizo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Ugavi na Uendeshaji wa MSD, Victor Sungusia, alibainisha maboresho yanayoendelea kufanywa na MSD katika nyanja mbalimbali kupitia majukumu yake ya uzalishaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji.

Sungusia alibainisha jinsi MSD ilivyojizatiti katika utekelezaji wa majukumu yake kupitia mifumo ya kisasa ya kidigitali, ugatuzi wa majukumu ya Kanda, ujenzi wa viwanda mbalimbali vya dawa na vifaa tiba, maboresho ya mfumo wa usambazaji wa bidhaa, upanuzi wa maeneo ya uhifadhi na kuwajengea uwezo watumishi wake.

Naye Meneja wa MSD Kanda ya Iringa, Robert Lugembe, akiwakiribisha wajumbe wa kikao hicho, alibainisha kuongezeka kwa uwezo wa MSD kuwahudumia wateja wake na kukidhi mahitaji, sambamba na maboresho ya upatikanaji wa bidhaa za afya mathalani vifaa tiba, mkoani humo.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


HII NI KERO

## Kutokuwepo viti kwenye vituo vya mabasi ya mwendokasi

BAADHI ya vituo vya mabasi ya mwendokasi, havina viti (mabenchi) ya kupumzikia abiria wanaosubiri usafiri huo tegemezi katika Jiji la Dar es Salaam. Tunashukuru kwa vituo vichache kama Kimara, Ubungo, Gerezani na Kivukoni kwa kuwepo huduma hiyo ingawa bado haikidhi mahitaji.

Ni muhimu kusambaza huduma hiyo katika vituo vingine hususan vile vinavyokusanya watu wengi kama Faya, Kimara Korogwe ili kuwasaidia abiria wenye mahitaji maalum wakiwemo wajawazito, wazee, wagonjwa na wenye ulemavu wa viungo.





MAONI YA MHARIRI

## Kutokomeza malaria nchini inawezekana

Ni taarifa zinazotia moyo kusikia kwamba wadau wa Mfuko wa Afya, wameichangia Serikali Sh. bilioni 37.7 kusaidia kutokomeza malaria nchini ifikapo mwaka 2030.

Wadau hao ni nchi za Uswisi, Denmark, Ireland, Korea Kusini, mashirika ya UNFPA, UNICEF na Benki ya Dunia.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema hayo wakati wa kikao chake na Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot.

Kwa mujibu wa Waziri, hatua hiyo inawanufaisha Watanzania wa pande zote mbili wanaokabiliwa na changamoto ya ugonjwa wa malaria, hasa wale wa vijijini na wale walio katika makundi hatarishi zaidi, hususani wajawazito, wazee na watoto.

Tunapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wadau hao kwa kutoa fedha hizo na pia tunaipongeza serikali yetu inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuendelea kuaminiwa na wada katika mapambano dhidi ya malaria hadi kuendelea kutoa fedha zao kwa ajili ya Watanzania.

Kimsingi, Tanzania imepiga hatua katika kupunguza ugonjwa wa malaria licha ya baadhi ya mikoa kuwa na maambukizi ya juu ya ugonjwa huo na mikoa mingine kama Arusha, Manyara, Njombe, Kilimanjaro na Iringa kuwa na maambukizi ya chini.

Mwezi uliopita, Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu, alisema kiwango cha maambukizi ya malaria nchini kimepungua na kufikia asilimia 8.1 mwaka 2023 kutoka asilimia 15 mwaka 2015.

Alisema kupungua kwa kiwango hicho cha maambukizi ya malaria kunatokana na jitihada za dhati za Serikali katika kuhakikisha kiwango cha malaria nchini kinafikia sifuri. Hii ni kwa kuweka mikakati ya kutokomeza mazalia ya mbu sambamba na kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi na dawa za kutibu malaria katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.

Wakati serikali ikifanya jitihada za kutokomeza malaria, wananchi pia tuna sehemu yetu ya kusaidia juhudi hizo na hatimaye kuharakisha maambukizi ya malaria nchini kubaki sifuri.

Baadhi ya mambo tunayopaswa kufanya ni kudhibiti wa mazingira yetu kwa kuhakikisha mbu na wadudu wengine waharibifu hawapati sehemu ya kuzaliana. Hii ni pamoja na kujitenga na maji yaliyotuama katika maeneon yetu na kufyeka vichaka na nyasi ndefu.

Lingine ni kutumia vyandarua vyenye dawa hasa kwa kuzingatia kwamba kimsingi mbu hupata wadudu wanaoambukiza malaria baada ya kumuuma mtu mwenye ugonjwa huo.

Wananchi tumekuwa wazembe kidogo katika kutumia vyandarua na badaa yake, hata katika maeneo ambayo watu wanagawiwa vyandarua bure, wengine huvigeuza kuwa neti za kuvulia samaki au huzungushia bustani za mbogamboga kuzuia kuku kama si kuanikia dagaa maeneo ya Kanda ya Ziwa.

Shime wananchi, malaria ni kati ya magonjwa yanayoua kwa wingi, tubebe jukumu letu kusaidiana na serikali kutokomeza ugonjwa huu.


### Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255753333330
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com


JICHO LANGU

## Dereva wa bodaboda heshimuni alama za barabarani si mapambo

JICHO langu leo linawaangazia madereva wa pikipiki za kubeba abiria maarufu kama bodaboda jinsi wanavyoshindwa kuheshimu sheria za usalama barabarani zikiwemo alama za barabarani.

Usafiri wa bodaboda kwa sasa, upo katika kila kona ya nchi na kwa hakika ni chanzo cha vijana wengi kujipatia vipato vyao vya kuendeshea maisha yao.

Wapo kila mkoa, wilaya, kijiji na hata vitongoji na usafiri wa bodaboda, umekuwa ukiwasaidia watu wengi mijini na vijijini.

Hata hivyo, licha ya umuhimu wake, madereva wengi wa vyombo hivyo vya moto vya magurudumu mawili, ndiyo wanaoongoza kwa kukiuka sheria za usalama wa barabarani na hivyo kuwa chanzo kikubwa cha ajali.

Ni nadra kumuona dereva wa bodaboda akisimama kwenye mataa hata kama hajaruhusiwa na hivyo kuhatarisha usalama wake, waenda kwa miguu na vyombo vingine vya moto.

"Taa za barabarani, zimewekwa kwa ajili ya madereva wa magari, siyo sisi bodaboda," mmoja wa madereva wa bodaboda, alijibu hivyo baada ya kupitisha pikipiki yake wakati taa nyekundu zinazoashiria kusimama, zikiwa zimewaka.

Jicho langu lilikuwa katika usafiri huo siku kadhaa zilizopita na lilimshuhudia dereva mmoja wa bodaboda, akipitiliza kwenye mataa bila kuzingatia taa za kuongoza magari barabarani.

> **Dhana kwamba bodaboda anayesimama kwenye mataa kwa kuzingatia sheria, ni ushamba, ni potofu na Jicho langu linaamini kwamba anayevunja sheria kwa makusudi, ndiye mshamba.**

Na Jicho langu lilipomhoji kwanini hakusimama pale taa zilipomtaka asubiri, dereva wa bodaboda alimjibu: "Taa za barabarani, zimewekwa kwa ajili ya madereva wa magari, siyo sisi wa bodaboda."

Jicho langu linawakumbusha madereva wote wa bodaboda umuhimu wa kuzingatia sheria za usalama wa barabarani.

Ieleweke kuwa alama za barabarani, hazikuwekwa kwa lengo la kupamba barabara, bali kuwasaidia wale wote waendesha vyombo vya moto na waenda kwa miguu.

Dhana kwamba bodaboda anayesimama kwenye mataa kwa kuzingatia sheria, ni ushamba, ni potofu na Jicho langu linaamini kwamba anayevunja sheria kwa makusudi, ndiye mshamba.

Madereva wengi wa bodaboda wamepoteza viungo vyao kama vile kukatwa miguu, mikono na kadhalika na wengine hata kuaga dunia, kutokana na kutozingatia sheria za usalama barabarani.

Ni vema sasa madereva wote wa bodaboda wakazingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima.

# TSC yatakiwa kutimiza azma ya Samia sekta ya elimu

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Zainabu Katimba, amewataka watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza azma ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuleta maendeleo katika Sekta ya Elimu.

Alisema hayo wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), unaofanyika jijini Dodoma.

Alileza kuwa TSC ndiyo yenye dhamana ya kusimamia walimu ambao wanachukua zaidi ya nusu ya watumishi wa umma nchini, hivyo ni vema kufanya kazi kwa bidii ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa amani na utulivu.

"Natumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati Rais Dk. Samia kwa kutimiza miaka mitatu tangu alipoanza kuliongoza Taifa la Tanzania…katika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia akitoa kipaumbele kikubwa katika Sekta ya Elimu, watumishi wa umma wamepandishwa vyeo kwa mfululizo," alisema.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Zainabu Katimba, akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), jijini Dodoma juzi.

Alisema katika kudhihirisha hilo, walimu 227,383 wamepandishwa vyeo na walimu 37,879 wameajiriwa katika kipindi cha uongozi wake.

"Ukiangalia juhudi hizo za Rais wetu, ni muhimu kwenu ninyi watumishi kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake kikamilifu na kusaidia kutatua changamoto zinazorudisha nyuma utendaji kazi wa walimu," alisema.

Aidha, Naibu Waziri ameipongeza TSC kwa kujenga mfumo wa kielektoniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS), kusimika mtandao wa intaneti kwenye baadhi ya Ofisi za Wilaya pamoja na kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la TSC makao makuu ambalo limefikia asilimia 37.

"Ninawapongeza kwa kuendelea kutekeleza majukumu yenu hususan katika masuala ya matumizi ya teknolojia ambayo yanarahisisha utekelezaji wa majukumu yenu. Kuhusu Mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi unaoendelea, ninamtaka Mkandarasi, SUMA JKT kuongeza kazi ya ujenzi ili kuhakikisha kazi hiyo inakamilika katika muda ulioainishwa kwenye mkataba," alisema.

Akizungumzia kuhusu Baraza la Wafanyakazi, Naibu Waziri Zainabu aliipongeza TSC kwa kuwa na Baraza la Wafanyakazi ambalo lipo hai huku akiwataka wajumbe wa Baraza hilo kutumia mkutano huo kuwalisisha vyema hoja za watumishi wengine ili zipatiwe ufumbuzi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

# 51 wachukua fomu kugombea uenyekiti

**Na Allan Vicent, Tabora**

WANACHAMA 51 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamechukua fomu ya kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa Mwenyekiti wa Mkoa huo, Mzee Hassan Mohamed Wakasuvi, aliyefariki dunia Februari 21, mwaka huu.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Mkoa, Idd Moshi, alisema kuwa jumla ya wana CCM 51 wamechukua fomu kwa ajili ya uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi hiyo.

Alisema zoezi la uchukuaji fomu lilianza Aprili 6, 2024 na kumalizika juzi saa 10.00 jioni ambapo hadi dirisha linafunguwa jumla ya makada 51 walijitokeza kuchukua fomu na kati yao wanne hawakurejesha fomu zao.

Mwenezi alifafanua kuwa kati ya makada 51 waliochukua fomu 45 ni wanaume na sita ni wanawake na miongoni mwao ni viongozi wa chama katika ngazi mbalimbali, viongozi wa serikali na wanachama wa kawaida.

Idd alisema kesho Kamati ya Usalama na Maadili ya chama ngazi ya mkoa itakutana kupitia majina ya wagombea wote na baada ya hapo, Aprili 13, mwaka huu, Kamati ya Siasa ya Mkoa itakutana na kutoa mapendekezo yao.

Alisema baada ya mchakato wa awali wa vikao vya chama ngazi ya mkoa, majina ya wagombea waliopendekezwa yatapelekwa makao makuu ya chama ili kuendelea na mchakato mwingine ikiwemo uteuzi wa mwisho wa wagombea.

"Uchaguzi ndani ya CCM ni wa kidemokrasia, kila mgombea ana haki sawa na mwenzake, naomba wagombea wote na wanaCCM tuendelee kuwa watulivu hadi vikao vya juu vitakapofanya uteuzi wa mwisho na kutuletea majina," alisema.

Aidha Mwenezi aliwataka wagombea kutofanya kampeni ya aina yoyote ile katika kipindi hiki hadi watakapoletewa majina na kutangazwa utaratibu wa uchaguzi huo ikiwemo tarehe ya uchaguzi na siku ya kuanza kampeni.

Alionya kuwa chama hakitasita kumchukulia hatua mgombea yeyote atakayefanya kampeni kinyume na utaratibu na jina lake linaweza kuondolewa katika orodha ya wagombea.

## Ulega: Chagueni wasioendekeza ugomvi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega, amewataka wanachama wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), kuchagua viongozi wenye nia ya kufanya kazi na kushirikiana na serikali kuleta maendeleo kwa wafugaji badala ya kuendeleza ugomvi wa mara kwa mara.

Waziri Ulega alisema hayo wakati akifungua mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama hicho unaofanyika jijini Dodoma jana.

"Chagueni viongozi watakaowaunganisha, waje kufanya kazi, washirikiane na serikali, chagueni viongozi wenye uelekeo uleule wa Serikali," alisema.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega

# MNH, ReSurge International kushirikiana upasuaji rekebishi

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) na Shirika lisilo la Kiserikali la Marekani ReSurge International, wamekubaliana kuendeleza ushirikiano na kujengeana uwezo katika kufanya upasuaji rekebishi.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Profesa Mohamed Janabi alisema hayo juzi baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Afisa Mkuu kutoka ReSurge International.

Alisema upasuaji huo ni kwa watu wenye changamoto mbalimbali ikiwemo waliopata ajali ya kuungua moto na wenye misuli iliyokakamaa kutokana na majeraha.

Profesa Janabi alisema Muhimbili ina nguzo tatu muhimu ambazo ni Huduma, Elimu na Utafiti, hivyo kama Hospitali ya Taifa haina budi kutekeleza kwa vitendo kwa kuwa ni wajibu wao.

Alieleza MNH itaendelea kuboresha ushirikiano na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi ili kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wake zaidi katika kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi hapa nchini.

"Ili kuendena na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika tiba, naamini katika kujifunza na kuongeza elimu kwa kubadilishana uzoefu kutoka kwa watua ambao wanajua zaidi," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Profesa Mohamed Janabi

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa MNH, Dk. Ibrahim Mkoma, alisema mwanzoni mwa mwaka huu MNH ilishirikiana na wataalam kutoka shirika hilo na kufanya kambi maalum ya siku tano iliyohusisha upasuaji wa urembo na upasuaji wa matibabu (Cosmetic and Reconstructive Surgery) kwa wagonjwa nane.

# Wanyama 9 wenye uwezo wa kuishi bila chakula, maji kwa muda mrefu



CHAKULA ndiyo chanzo kikuu cha nishati kwa mwili wa ili kufanya kazi vizuri.

Wanadamu hawawezi kuishi bila chakula na maji kwa siku nyingi. Ulaji chakula ni sehemu ya maisha ya binadamu na ni asili ya binadamu kula chakula kila siku. Lakini, je, unajua kwamba kuna viumbe wengi wanaoweza kuishi bila kula chakula au kunywa maji?

Wanyama wengine wanahitaji kula mara kadhaa kwa siku ili kupata nguvu ya kuishi. Kwa mfano, tembo anaweza kula hadi kilo 375 za mimea kwa siku.

Kando na ngamia ambao wanaweza kuishi kwa miezi kadhaa bila maji, kuna wanyama wengine wanaofanana na ngamia.

Baadhi ya wanyama hao ni:-

**1. Mamba**

Mamba, ambaye ni mmoja wa viumbe wa zamani zaidi duniani, anaweza kuishi kwa miezi kadhaa bila chakula na wakati mwingine katika hali mbaya, anaweza kuishi hadi miaka mitatu bila chakula.

Wanahifadhi nishati kwa kupunguza harakati na wakati mwingine huacha kabisa kusonga.

**2. Chura**

Chura hupatikana zaidi kwenye maeneo yenye unyevunyevu na miili yao inaweza kukaa bila chakula kwa hadi miezi 16.

**3. Buibui**

Buibui wanapaswa kusubiri chakula chao kufika na wakati mwingine kusubiri kunaweza kuwa kwa muda mrefu.





Miili ya wadudu hawa, imeundwa kwa namna ambayo wanaweza kukaa kati ya miezi mitatu hadi minne bila chakula na hata hadi mwaka mmoja.

**4. Kobe**

Kobe ni mojawapo ya wanyama wanaoishi kwa muda mrefu zaidi wa aina yake. Kobe mkubwa mwenye uzito wa hadi kilo 417, anaweza kuishi bila chakula na maji kwa mwaka mzima.

**5. Simba wa baharini**

Simba wa baharini wanaweza kuishi bila chakula kwa muda wa wiki nane hadi 10, lakini jambo la kushangaza ni kwamba wasipokula, huwa hai wanapoanza kazi yao ya kuwinda.

**6. Nyoka**

Nyoka wanaweza kuishi bila chakula kwa zaidi ya mwaka mmoja. Hii inawezeshwa na ukweli kwamba mfumo wao wa utumbo, hupungua kwa asilimia 70 katika hali ya hewa ya baridi.

**7. Nge**

Nge hula theluthi moja ya uzito wa mwili wao kwa mlo mmoja. Hii husaidia tu kupunguza kemia ya mmeng'enyo wa chakula na kudhibiti lishe yao na kuifanya iwe rahisi kwao kukaa bila chakula kwa mwaka.

**8. Nyangumi**

Nyangumi hutumia mafuta ya ziada wanayohifadhi kila wanapokula wakati wa msimu wa joto, jambo ambalo huwawezesha kukaa bila chakula kwa hadi miezi sita.







Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Aprili 10-16, 2024 |




Jarida hili haliuzwi

# Muungano ulivyoimarisha ukaribu kiuchumi, kijamii




UK. 12 & 13

# ‘Mafundi’ kutengeneza migogoro washughulikiwe



**Na John Ngunge**

*“NIDHAMU ya kazi, ni msingi, wa mafanikio mema kazini. Viongozi na wafanyakazi, lazima wote, tuwe na nidhamu. Migogoro na migongano ya kazini ni ukosefu wa nidhamu.*

*“Viongozi wote wajibu wenu mkubwa, ni kulinda heshima, na kudumisha nidhamu ya kazi.”*

*Maneno hayo kuntu yamo kwenye kibao kilichopigwa miaka ya nyuma na Bendi ya JUWATA Jazz Band iliyokuja kujuliana baadaye kama OTTU Jazz.*

Ni bendi iliyokuwa inamilikiwa na Jumuiya ya Wafanyakazi, sasa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA).

Maneno yaliyomo kwenye wimbo huo yana ujumbe muhimu hadi leo kwani sumu ya utendaji mbovu ni kukosekana kwa nidhamu ya kazi. Kwamba kunapokuwa na migogoro na migongano kazini, hatuwezi kutegemea ufanisi katika eneo hilo.

Wimbo unawakumbusha viongozi kwamba wajibu wao mkubwa ni kudumisha nidhamu ya kazi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hakuna migogoro na migongano katika maeneo ya kazi wanayoyaongoza. Je, hali ikoje?

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan hivi karibuni alitoa onyo kwa wateule wake akiwataka kwenda kutatua migogoro katika maeneo yao na kamwe wasiwe sehemu ya utengenezaji wa migogoro.

Rais Samia amerudia kutoa onyo hilo baada ya kuwa amechukua hatua kali dhidi ya baadhi ya wateule wake waliotengeneza migogoro katika taasisi au maeneo wanayoyaongoza.

Migogoro kati ya wateule/watendaji katika sekta ya umma imekuwa ikikwamisha utendaji kazi. Kama Waswahili wanavyosema, mafahali wawili wanapogombana zinazotumia ni nyasi na katika muktadha huo kunapokuwa na mgogoro kwenye ofisi ya umma, wanaoumia ni wananchi kwa kukosa huduma stahiki.

Ajabu, watu wameendelea kutengeza migogoro wakiwemo wateule wa Rais licha ya ukweli kwamba wanaobainika, hatua kali za kinidhamu zimekuwa zikichukuliwa dhidi yao. Hatua hizo ni kama kutengua uteuzi wao, kuonywa, kusimamishwa kazi na zingine nyingi.

Rais Samia amewataka viongozi wateule kuwa sehemu ya kuwaunganisha watu na sio kutengeneza migogogoro katika jamii yao.

Kwamba wanapaswa kuwa watatuzi wa migogoro kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo wakitumia pia busara, na kushirikisha wataalamu wa fani mbalimbali katika eneo au ofisi zao, yaani washauri wataalamu na jamii.

Suala la kuwepo kwa migogoro katika baadhi ya ofisi za umma lina athari nyingi na halipaswi kufumbiwa macho. Linadumaza jitihada za serikali kuwaletea maendeleo wananchi.

Migogoro mingi inayokuja kutokana na majukumu ya kazi hutengenezwa na mtu, jamii au kikundi cha watu na kusukumizwa katika idara au ofisi za umma au binafsi, ili wahusika wahangaike nayo.

Akiwaapisha viongozi wateule, Aprili 4, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, Rais Samia aliwataka kwenda kufanya kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi, kutatua migogoro yao na siyo kwenda kutengeneza migororo.

“Niwaombe kafanyeni kazi kwa kuwaunganisha watu, nendeni katatueni migogoro iliyoko huko mnakokwenda na msiende kutengeneza migogoro,” alionya.

Onyo la Rais Dk. Samia limekuja takribani miezi 10 hivi baada ya kutengua uteuzi wa viongozi wakuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Juni 18, mwaka jana.

Akiwaapisha wateule wapya wa RITA, Samia alibainisha kuwa ugomvi usiokwisha uliohushisha utendaji kazi katika ofisi ya RITA ndiyo ulikuwa chanzo ya utenguzi huo.

“Kabidhi Wasii Mkuu na naibu wako nimewateua baada ya kuwaondoa viongozi wote wawili waliokuwepo pale. Nilikuwa nategemea wananchi wapate huduma za kuridhisha ndani ya ile ofisi, lakini kilichokuwa kinatokea ilikuwa ni ugomvi.

“Nikasema labda kwa kuwa wote walikuwa akina mama ndiyo maana kulikuwa na ugomvi mkubwa, lakini ukiangalia kwa ndani kulikuwa na kutokutekelezeka kwa kazi vizuri, mwingine akisema huyu anakasirika, mwingine akirekebisha mwingine anachafua, kwa hiyo nikaamua kuwaondoa wote wawili watapangiwa kazi nyingine, sasa nendeni ninyi,” Rais aliwaagiza wateule wapya.

Aliwataka wakashirikiane kutoa huduma kwa wananchi akisema: “Ile ni ofisi kubwa, wananchi wanaitegemea, badala ya kujenga ugomvi humo ndani, nendeni kashirikianeni, angalieni wapi kumeharibika, wekeni sawa toeni huduma.”

Rais Dk. Samia alieleza kulikuwa na baadhi ya kesi ambazo zilifika ofisini kwake na kila alipojaribu kuwaambia walalamikaji warudi Rita, walikataa wakisema hapaendeki na hawajui kinachoendelea.

“Kama mlivyokula kiapo hapa mkashirikiane, nimewateua kuhakikisha mambo yanakuwa sawa,” alisema.

Hatua ya Samia ni mwendelezo wa hatua kama hiyo iliyokuwa ikichukuliwa na Rais Dk. John Pombe Magufuli enzi za uhai wake kwa kuwatumbua wateule ambao walikuwa wakitengeneza migogoro mara kwa mara.

Mteule mmoja aliyepata kuwa Mkuu wa Mkoa Mwanza alitumbuliwa kwa kile kilichodaiwa kutengeneza migogoro ya mara kwa mara.

Kama hiyo haikutosha siku ya kuwaapisha wateule Juni 20, 2020, Magufuli alisema haridhishwi kuona migogoro baina yao.

“Niseme kwa ufupi sana, nendeni mkazingatie viapo vyenu. Inanisikitisha pale ninapowateua na watu hawafuati viapo vyao.

“Utakumbuka hivi karibuni Arusha ilibidi nitengue uteuzi wa wote niliokuwa nimewateua kuanzia RC, Mkurugenzi pamoja na DC. Ni kwa sababu katika kipindi cha karibu miaka miwili walikuwa wanagombana tu, kila mmoja ni bosi, kila mmoja anatengeneza mizengwe ya mwenzake. Waliniudhi,” alisema.

Katika jamii zetu wapo watu mafundi wa kutengeneza migogoro na kuisukumiza katika jamii au ofisi fulani. Hao nao wanahitaji kumulikwa.

Suala la kuzalisha/kutengeneza lipo pia kwa watumishi wa ngazi ya mwanzo kabisa serikalini, yaani maafisa watendaji wa vijiji. Baadhi yao wanashutumiwa kuwa sehemu ya migogoro katika taasisi zilizopo kwenye maeneo yao, wakipika majungu, kuwagawa wanavijiji katika hoja ambazo wamezitengeneza na ili kuzihalalisha wanaitisha mikutano ya kijiji kukubaliana na hoja zilizopikwa.

Wapo maofisa watendaji wa vijjiji na wa kata ambao maeneo fulani wanawaitwa ‘miunguwatu’ wanakwamisha shughuli za kuwaletea maendeleo wananchi wa maeneo hao.


Katika mazingira mengine, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, Februari 14, mwaka jana, alibainisha hilo alipotoa onyo; “msijifanye ‘miungu watu’ kwa kuwakamata wananchi na kupora mali zao kwa uonevu, simamieni sheria lakini msionee watu. Sisi huku juu tunaletewa tuhuma nyingi za ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma ambazo zinafanywa na baadhi yenu Maofisa Watendaji wa Kata,” alisema.

Aliwataka wakurugenzi wote nchini kufuatilia tuhuma hizo na kuchukua hatua stahiki za kisheria na kinidhamu.

Taarifa zinaonesha kuwa yapo maeneo ya vijiji katika baadhi ya halmashauri ambazo wananchi wake wamewakataa watendaji wa vijiji wanaodumaza maendeleo katika taasisi zilizopo katika maeneo yao kwa kutengeneza migogoro isiyoisha kwa wananchi.

Ni vema wakurugenzi watendaji wa halmashauri wakachukua hatua stahiki za kuwawajibisha maafisa watendaji wa vijiji wanaotengeneza migogoro kama ambavyo Rais Dk. Samia anavyowawajibisha wateule wake wanaotengeza migororo maeneo ya kazi.

La kuzingatia ni kwamba, watu mnaweza msiwe marafiki. Mnaweza kuwa na mitazamo inayosigana sana na hata mnaweza kuwa maadui kabisa! Lakini mnapoingia ofisi ya umma (hata ya binafsi) uadui wenu mnauacha nje, mnashirikiana kwa kuzingatia nidhamu ya kazi kutoa huduma kwa wananchi. Mkitoka nje ya ofisi mnaendeleza uadui wenu alimradi usiguse misingi ya kazi na maslahi ya wananchi.



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Maadhimisho miaka 30 mauaji Rwanda yatukumbushe kuchunga amani yetu



NCHI ya Rwanda mwishoni mwa wiki imeadhimisha miaka 30 tangu kutokea kwa mauaji ya kimbari baina ya Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani yaliyojiri mwaka 1994.

Ni kumbukumbu iliyoadhimishwa katika Jiji la Kigali na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka barani Afrika, Ulaya, Amerika na Asia ikiwa ni pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan.

Ishara ya kuanza kwa kumbukumbu ya mauaji ya kimbari ilikuwa pamoja na kuwasha mishumaa katika eneo la Gisozi, mahala ambapo mabaki ya miili ya watu zaidi ya 250,000 imezikwa katika kaburi la pamoja.

Mauaji hayo ya kimbari yalianza April 7, 1994, siku moja baada ya ndege iliyombeba Rais wa wakati huo wa Rwanda, Juvenali Habyarimana na aliyekuwa Rais wa Burundi, Cyprian Ntyaramira kutunguliwa wakati ikijiandaa kutua katika Uwanja wa Ndege wa Kigali. Viongozi hao walikuwa wakitokea Tanzania walikokuwa na Mkutano na Rais Ali Hassan Mwinyi.

Baada ya tukio hilo, majeshi ya serikali ya wakati huo na makundi yenye silaha ya Impunzamugambi na Intarahamwe yaliyokuwa na unasaba na chama tawala cha MRND yalianza kuwaua watu wa jamii ya Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani wakilenga kumaliza kabisa kizazi chao (ethnic cleansing).

Mtu mmoja ambaye alifanikiwa kutoroka akiwa na umri wa miaka sita baada ya kushuhudia mauaji ya ndugu zake anasema ilifikia wakati wakajua fika kwamba hakuna eneo ambalo lilikuwa salama jijini Kigali.

Hata alipojiunga na msafara wa watu waliokuwa wanakimbia alipoteana na ndugu zake wachache waliokuwa wamebaki akiwemo mmoja wa wazazi wake.

"Kwa hiyo, tukaamua kujiunga na wengine waliokuwa wakiondoka huko, wakijaribu kuepuka vizuizi vya barabarani ambavyo vilisimamiwa na wapiganaji waliojihami kwa mapanga. Tulihisi kana kwamba mji mzima wa Kigali ni mauaji tu. Hakuna aliyekuwa na uhakika wa kufika salama huko tunakokimbilia. Tulikuwa maelfu ya watu, sote tukitembea kwa miguu, au kutumia baiskeli na pikipiki, magari, au malor," anasema mtu huyo ambaye ni miongoni mwa wachache waliofanikiwa kuepuka kifo alipozungumza na Shirika la Utangazaji la Uingereza hivi karibuni.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, karibu watu milioni moja waliuawa hadi kufikia mwezi Julai ambapo vikosi vya vuguvugu la Ukombozi wa Rwanda (Rwanda Patriotic Army (RPA) vilipofanikiwa kukomesha mauaji hayo baada ya kuudhibiti mji wa Kigali.

### SABABU YA MAUAJI

Mauaji hayo yalitokea kutokana na sababu mbalimbali lakini kubwa ikiwa ni ubaguzi wa kikabila (ubaguzi wa rangi) baina ya Watutsi na Wahutu.

Hali ya mvutano baina ya makabila hayo ulikuwa umetanda kwa miongo kadhaa. Tatizo lilianzia kwa Wakoloni wa Kibelgiji waliokuwa wakitawala Rwanda kuendesha siasa za 'wagawe ili utawale' ambao ndio walichochea ukabila. Ubelgiji ilitawala nchi hiyo baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia hadi mwaka 1962.

Wabelgiji waliwaona Watutsi walio wachache kuwa bora, na kuwapendelea katika nafasi za uongozi kulinganisha na Wahutu walio wengi. Baadhi ya Watutsi wenye madaraka nao wakaonesha waziwazi kuwabagua Wahutu. Upendeleo huu ulizua mvutano na malalamiko muda wote.

Mwishoni mwa miaka ya 1950 na mwanzoni mwa miaka ya 1960, mapambano ya kudai uhuru kutoka kwa utawala wa Ubelgiji yalipata nguvu nchini Rwanda. Mapambano haya yalihusisha makundi mawili hasimu ya Wahutu na Watutsi huku makundi hayo mawili yote yakitafuta kumng'oa mkoloni ingawa yenyewe kwa yenyewe yalikuwa yakipingana!

Mapinduzi ya 1959-1962 yalisababisha mkoloni kuachia madaraka na Rwanda kupata uhuru, lakini viongozi wa Wahutu ndio walichukua udhibiti wa serikali.

Watutsi wengi waliuawa katika mapinduzi hayo au kulazimishwa kuikimbia nchi yao huku serikali mpya ya wazawa ikionesha waziwazi chuki na vitisho kwa Watutsi.

Inaelezwa kwamba takribani Watutsi zaidi ya 336,000 walilazimika kutafuta hifadhi katika nchi jirani. Kundi la wakimbizi hawa lililoelekea nchini Uganda likiaamua kuanzisha Rwanda Patriotic Front (RPF) ambayo, chini ya uongozi wa Fred Rwigyema na Paul Kagame, likawa jeshi lililo tayari kwa vita dhidi ya Serikali ya Kigali.

Rwanda iliendelea kutawaliwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vilipiganwa kati ya wanajeshi wa Rwanda, wakiiwakilisha serikali ya nchi hiyo, na waasi hao wa Rwandan Patriotic Front (RPF) kuanzia Oktoba 1, 1990 hadi 18 Julai 1994.

Kwa hiyo, cha msingi hapa ni sumu ya ukabila iliyojengwa na wakoloni ndiyo ambayo imekuwa ikiitafuna Rwanda.

### MADHARA YA KUBAGUANA

Madhara ya ukabali, kama ambavyo tumeona yalisababisha kuzaliswa kwa wakimbizi kutoka kabila la Watutsi baada ya Wahutu walio wengi kuchukua madaraka ya kuongoza nchi katika mapinduzi ambayo pia yalimwaga damu nyingi ya Watutsi.

Lakini baya zaidi ni hayo mauaji ya kimbari ambayo wauaji walipania kufuta kabisa kizazi cha Watutsi walio wachache. Hali hii ikisababisha nchi jirani kuanza kubeba mzigo wa wakimbizi.

Katika kitabu cha Safari ya Maisha Yangu kilichoandikwa na Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi ameeleza namna serikali yake ilivyokuwa ikishughulikia wakimbizi kutoka Rwanda waliokuwa wakimiminika kila siku nchini, hususani katika Wilaya ya Ngara mkoani Kagera.

Lakini mbali na mauaji ya kimbari ambayo yameacha madonda na maumivu, nchi ya Rwanda imekuwa haina utulivu kwa muda mrefu.

Hali ya usalama ilikuwa mbaya zaidi katika tawala zilizopita lakini hata sasa bado kuna vikundi vya Wahutu ambavyo haviridhiki na utawala wa Kigali.

Hata hivyo, Rais Paul Kagame anapaswa kupewa maua yake angali hai kwani katika kipindi cha miaka 30 amejitahidi kujenga mshikamano na kuaminiana miongoni mwa Wanyarwanda, hatua ambayo imesaidia sana katika kuwaletea Wanyarwanda maendeleo makubwa.

Miaka 30 sasa, Wanyarwanda kupitia kaulimbiu yao iitwayo Kwibuka, wameendelea kuinuka na chini ya uongozi wa Rais Kagame, Rwanda imeibuka kutoka kuwa Taifa lililofeli na kuwa sehemu ya matumaini kwa maisha ya binadamu.

### CHA KUJIFUNZA

Watanzania tunachopaswa kujifunza hapa ni kuendelea kulinda amani yetu na kuepuka vitu ambavyo vinaweza kutugawa na kusababisha chuki miongoni mwetu. Mambo yanayoweza kutugawa ni ukabila, udini, umajimbo na hata itikadi za kisiasa kama wanasiasa wetu hawatakuwa makini na ndimi zao.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kututahadharisha kuhusu kulea ubaguzi wa aina yoyote ile, uwe wa kikabila, umajimbo, udini, rangi na kadhalika akisema dhambi ya kumbagua mwananchi mwenzako ni sawa na kula nyama ya mtu. Haiwezi kukuacha salama.

Kwa hiyo, tunapaona yeyote miongoni mwetu anaonesha dalili za kuleta jambo linalotugawa kama Watanzania, tumkemee kama pepo mchafu na tusimruhusu kupandikiza hiyo chuki.

### FALSAFA YA R4 ZA SAMIA

Nichukue fursa hii kumpongeza Rais Samia kuja na Falsafa ya R4 inayoonesha kwamba Tanzania tuna kiongozi aliyedhihirisha anajua umuhimu wa kuleta umoja, mshikamano na amani ya nchi.

Hizo 'R' nne ni vifupi vya maneno ya Kiingereza; Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko/mageuzi) na Rebuilding (Kujenga upya).

Mambo haya yote ambayo Rais Samia anayetekeleza kwa vitendo ni kitu muhimu katika ujenzi wa taifa ili kuwa na sauti moja. Rais Samia anaamini maridhiano na maelewano yanawezekana kwa kukaa pamoja na kujadiliana kwa njia ya mazungumzo na ya amani na hivyo kuhakikisha umoja wa Watanzania unaendelea kuimarika.

Shime Watanzania, wakati tukijifunza tatizo la kulea ubaguzi kutoka kwa majirani zetu wa Rwanda, ni vyema tuendelee kuimarisha amani ya nchi yetu na kumuunga mkono Rais Samia katika kufanyia kazi falsafa yake hiyo ya 'R' nne.

# Muungano ulivyoimarisha ukaribu kiuchumi, kijamii




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizindua nembo ya kaulimbiu ya maadhimimisho ya sherehe za miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma.

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Jumatatu ya wiki hii amezindua nembo na kaulimbiu ya maadhimimisho ya sherehe za miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uzinduzi uliofanyika Jijini Dodoma.

Kaulimbiu inasema: "Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Tumeshikamana, Tumeimarika kwa Maendeleo ya Taifa letu."

Itakumbukwa kwamba Tanganyika na Zanzibar viliungana rasmi na kuzaliwa Tanzania Aprili 26, 1964.

Katika uzinduzi huo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anawataka Watanzania wote, Bara na Visiwani waendelee kuulinda, kuuenzi, kujivunia na kuuthamini Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Waziri Mkuu anasema Muungano huu ni tunu adimu na adhimu inayopaswa kulindwa kwa gharama yoyote na hivyo anamtaja kila mtanzania awe mlinzi wa huu muungano.

Waziri Mkuu anasema anasema Watanzania wana kila sababu ya kujivunia muungano wao huu kutimiza miaka 60.

"Ni ukweli usiopingika kwamba muungano wetu umeendelea kuwa na tija kubwa na kuchagiza maendeleo ya nchi yetu na wananchi wote kwa ujumla," anasema Majaliwa na kuongeza kwamba kilele cha sherehe za Muungano kitafanyika katika Uwanja wa Uhuru, Jijini Dar es Salaam na hivyo anatoa wito kwa wananchi wote wa pande mbili za muungano wajitokeze kwa wingi ili kushuhudia maadhimisho hayo.

## TUWASHUKURU WAASISI

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tunaojivunia kutokana na faida zake lukuki kama makala haya yanavyoeleza, ni matokeo ya fikra zilizoasisiwa na Mwalimu Nyerere kwa upande wa Tanzania Bara na Abeid Aman Karume kwa upande wa Zanzibar.

Waasisi hawa wa muungano hawapo tena duniani lakini muungano umeendelea kudumu.

Serikali zote, ikiwemo hii ya Awamu ya Sita zimekuwa zikifanya jitihada kubwa kuimarisha Muungano huu wa mwaka 1964 kwa bahati Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inasisitiza umuhimu wa kudumisha Muungano.

## MUUNDO WA MUUNGANO

Muundo wa Muungano wa Tanzania kama ulivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, una vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji ambavyo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ambavyo ni Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Zanzibar; na vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ambavyo ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Visiwani.

## SABABU YA MUUNGANO

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umekuwepo kutokana na sababu mbalimbali kama vile kuwepo kwa mahusiano ya karibu na ya kihistoria baina ya Tanganyika na Zanzibar katika nyanja mbalimbali kama vile undugu wa damu, biashara, utamaduni, lugha na mahusiano ya karibu kisiasa hususani baina ya vyama vya TANU na ASP.

Pia, azma ya kuwa na Muungano wa Afrika, hususan kwa kuanzia na Shirikisho la Afrika Mashariki. Hata kabla ya uhuru wa Tanganyika, Mwalimu Nyerere pamoja na viongozi wengine waliokuwa wakipigania uhuru katika ukanda wa Afrika walikuwa na matarajio ya kuwa na Muungano wa Afrika. Mwalimu Nyerere binafsi alipendelea uwepo Muungano wa Afrika kwa kuanzia na Mashirikisho ya kikanda.

Kimsingi zipo sababu mbalimbali zilizosababisha Muungano huu kama vile historia za nchi hizo mbili, ukaribu wa nchi hizi mbili, muingiliano wa kijamii, ushirikiano wa kibiashara, ushirikiano madhubuti na wa muda mrefu wa kisiasa baina ya TANU na ASP, ushirikiano na urafiki wa muda mrefu kati ya watu, viongozi, na wakati wa harakati za utaifa uliopelekea uhuru wa nchi hizo mbili.

## FAIDA ZA MUUNGANO

Kupitia muungano, hakuna ubishi kwamba wananchi wa pande zote mbili za Muungano wameongeza ukaribu wao kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Ukaribu huo unatokana na juhudi za serikali zote mbili, ya Muungano na ile ya Zanzibar kuweka mazingira wezeshi kupitia mazungumzo yenye lengo la kutatua changamoto zinazoukabili Muungano.

Kamati ya pamoja ya kujadili changamoto za muungano iliyo chini ya ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imekutana mara kwa mara na kujadili changamoto za muungano kwa ufanisi.

Hata wizara na sekta nyingine zisizo za Muungano zimekuwa pia zikikutana na kujadili namna ya kushirikiana katika kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.



Biashara ya picha na sanaa mbalimbali Zanzibar.



Biashara katika mitaa ya Kariakoo.




Shughuli za uvuvi katika bahari ya Hindi.

Kimsingi, vikao hivi vimekuwa vikiimarisha ushirikiano wa pande zote mbili na kuwaweka watendaji karibu zaidi.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Suleiman Jafo alisema kwamba tangu mwaka 2006, hoja 22 kati ya 25 zilipokewa na Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye kwenye orodha ya hoja za muungano.

Jafo anataja kero zilizobaki kuwa ni suala la mgawanyo wa mapato yatokanayo na hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, mgawanyo wa faida kutoka Benki Kuu, suala zima la uingizwaji wa sukari inayozalishwa katika kiwanda cha Mahonda, Zanzibar katika soko la Tanzania Bara pamoja na usajili wa vyombo vya moto.

Jafo anasema hoja hizo zilizobaki ziko katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi. Anasema kwa kuwa serikali zote mbili, SJMT na SMZ zina nia na dhamira ya dhati ya kuhakikisha mambo yote yanayoleta changamoto katika utekeleaji wa masuala ya muungano yanapatiwa ufumbuzi, basi hata hizo chache zilizobaki zitapatiwa ufumbuzi.

Anasisitiza kwamba Serikali za pande mbili chini ya uongozi wa Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Sulihu Hassan na Serkali ya Awamu ya Nane Zanzibar zimeweka suala la kuimarisha muungano kuwa ni moja ya vipaumbele vyao na hivyo zinaendelea kushirikiana kwa pamoja kuhuisha na kudumisha muungano.

**HOJA ZILIZOPATIWA UFUMBUZI**

Baadhi ya changamoto zilizopatiwa ufumbuzi ni pamoja na utekelezaji wa sheria ya tume ya haki za binadamu na utawala bora, uvuvi kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu, utekelezaji wa sheria ya usafiri wa majini pamoja na mgawanyo wa mapato ya misaada na uwezo wa Zanzibar kukopa.

**MUUNGANO UKO IMARA**

Mwaka huu wa 2024, Muungano wa Tanzania ulitimiza miaka 60 ukiwa umefanya mambo mengi makubwa kwa manufaa ya pande mbili za muungano.

Matarajio ya Watanzania wengi ni kwamba muungano ambao ni wa wananchi utaendelea kuimarika zaidi na wananchi wa pande zote mbili kutumia fursa nyingi za uchumi zinazopatikana pande zote mbili za Muungano kujiletea maendeleo.

Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete aliwahi kusema kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uko imara na kwamba utaendeleaa kuzidi kuwa imara kwa wakati huu na hata hapo baadae.

Kikwete anasema kuwa sherehe za muungano ambazo zilikuwa za mwisho kwake akiwa madarakani, zilionyesha ukomavu wa muungano licha ya kuwepo kwa changamoto chache sana ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi kuhusiana na Muungano.

Anasema juhudi za makusudi zimekuwa zikichukuliwa katika kuhakikisha changamoto zilizopo zinapatiwa ufumbuzi.

Kikwete anazidi kusema manufaa makubwa ambayo watu wameyapata katika muungano, ni kujuana kati ya Wanzanzibari na Watanganyika katika unyonge na kuongeza heshima ya uhuru na nguvu kushika serikali.

Faida za muungano siku hizi zinaonekana pia katika nyanja za kiuchumi na kijamii. Kwamba kuna Watanzania wengi siku hizi ambao wanafaidika na muungano kwa kufanyakazi, kulima, au kufanya bishara katika sehemu moja yapo ya muungano ambako si asili yao kwa kuzaliwa.

Lakini moja ya faida za kijamii imekuwa ni watu wa maeneo haya mawili ya nchi yetu kuoleana bila tatizo kulinganisha na pale Mtanzania anapotaka kuoa ama kuolewa katika nchi kama Rwanda au Kenya.

**HASARA ZA KUTOKUWEPO MUUNGANO**

Muungano usingekuwepo, kusingekuwa na faida tunazozizungumza leo kama hizo za ushirikiano wa kindugu.

Lakini kungekuwa na hasara kubwa kwa pande zote, Tanganyika na Zanzibar kwamba Zanzibar ingedumu katika wasiwasi kwani mbinu zingeweza kutumika kumrudisha Sultani huku Tanganyika, pamoja na ukubwa wake, isingekuwa salama kabisa kama kungekuwa na vurugu visiwani.

**UHALALI WA MUUNGANO**

Baada ya kuundwa kwa serikali mpya ya ASP ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar iliyokuwa ikiongozwa na Baraza la Mapinduzi chini ya Mwenyekiti Abeid Karume, viongozi wa Tanganyika na Zanzibar walianza mazungumzo ya kuungana.

Mazungumzo hayo yalikuwa ni ya kuungana kwa msingi ya kurudisha undugu na umoja wa watu wa Zanzibar na Tanganyika, kama vile ilivyokuwa kabla ya ukoloni kugawana bara hili na kutawala Afrika.

Mazungumzo hayo yalifanyika Dar es Salaam na yalifanyika kwa lengo la kuweka msingi ili wataalamu wakayaandike hayo makubaliano katika lugha ya kisheria.

Aprili 22, 1964 Mwalimu Nyerere, Rais wa Tanganyika aliienda Unguja kukamilisha mazungumzo yake na viongozi wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wakafikia makubaliano.

Kwenda kwa Mwalimu Nyerere Zanzibar kukawa kama kugonga muhuri katika maafikiano ambayo yalikuwa yapo tangu zamani. Baada ya hapo, Nyerere aliitisha kikao cha dharura cha Bunge la Tanganyika Aprili 25, 1964.

Kikao hicho kikathibitisha makubaliano ya msingi juu ya muungano yaliyofikiwa katika mazungumzo baina ya viongozi wa Tanganyika na Zanzibar na kwenye hotuba yake Nyerere alisisitiza umuhimu wa kuunganisha nchi mbili jirani ambazo kabla ya hapo ziliwahi kuwa nchi moja.

Aprili 26, mwaka 1964 Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ilizaliwa na baadaye ikapewa jina Tanzania, na siku hiyo hiyo Karume akifuatana na mawaziri na wajumbe wa Baraza la Mapinduzi walikwenda Dar es Salaam kutia saini hati ya Muungano.



# Maajabu ya tunda fenesi linavyoweza kutibu aina tatu ya saratani na moyo

FENESI au kwa jina la kisayansi Artocarpus heterophyllus, ni tunda la kitropiki ambalo hukua Asia, Afrika na Amerika Kusini na linajulikana kuwa tunda kubwa zaidi linaloweza kuliwa ulimwenguni.

Mbegu na nyama ya tunda hili, inaweza kuchemshwa na kuliwa katika kama kari; tunda likiiva kabisa linaweza kuliwa likiwa bichi na kutumika katika vyakula vitamu na vilivyo chachu.

Barani Afrika, tunda hili huliwa mara nyingi likiwa limeiva, lakini katika Bara Asia, linaliwa kama mbadala mzuri wa nyama katika matoleo ya mboga mboga ya mapishi ya asili kama vile nyama ya kuku.

Ingawa, badala ya nyama maarufu, fenesi haichangii kiwango sawa cha protini, kwa hivyo ni wazo zuri kuichanganya na viungo vingine vya protini kutoka kwa mimea kama vile maharage, kunde na njugu .

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO), sasa limeorodhesha tunda hili la fenesi kama mojawapo ya mazao yaliyosahaulika barani Afrika ambayo yanaweza kusaidia kumaliza njaa na pia kupambana na aina mbalimbali ya maradhi.

**ZIFUATAZO NI BAADHI YA FAIDA ZA TUNDA HILI:**

**Kinga dhidi ya magonjwa**

Fenesi ni chanzo muhimu cha aina mbalimbali za phytonutrients, misombo hii ya mimea, ni kinga na inaweza kusaidia kuzuia maendeleo ya baadhi ya magonjwa sugu, kama vile kisukari. Ina vitamini C, carotenoids pamoja na polyphenols na flavonoids.

Hutumika katika matibabu ya saratani ya tezi dume, saratani ya tumbo, saratani ya mapafu, magonjwa ya moyo na shinikizo la damu. Pia ina uwezo wa kuzuia mtu kuzeeka.

**Chanzo cha vitamini na madini**

Fenesi ina kiasi cha chini cha kalori wakati, kulingana na angalau utafiti mmoja ina virutubisho vingi zaidi kuliko matunda mengine mengi maarufu kama vile tufaha, parachichi na ndizi. Kwa kweli, mbegu na nyama yake ina kalsiamu na chuma zaidi kuliko matunda mengine ya kitropiki na ni chanzo muhimu cha vitamini B ikiwa ni pamoja na B1, B3, B6 na folate.

**Inaweza kusaidia kuboresha afya ya moyo**

Pamoja na kusambaza phytonutrients ya kinga fenesi pia ina virutubisho rafiki kwa moyo ikiwa ni pamoja na potasiamu na nyuzi.

**Kuboresha kinga ya mwili**

Ni viungo vya nyuzi katika tunda hili zinazosaidia utumbo pamoja na vitamini C na beta-carotene ambayo yanapendekeza kwamba fenesi inaweza kusaidia afya ya kinga na uwezekano wa kupunguza hatari ya kuambukizwa na virusi.

Mbali na hayo, kiungo kilichopatikana katika mbegu ya matunda, kinaonekana kuamsha seli muhimu za kinga, zinazoitwa neutrophils. Seli hizi za kinga ni mojawapo ya mistari yetu ya kwanza ya ulinzi na huongeza nguvu za seli nyingine za kinga.

**Kutengeza bidhaa nyingine**

Kando na kutumika katika kuoka na kutengeneza sharubati na saladi. Fenesi inaweza kupikwa ikiwa kijani. Mbegu zinaweza kupikwa au kuliwa zikiwa mbichi.

Pia fenesi hutengeneza pipi, ice cream, juisi, mvinyo, jamu na kachumbari.

Majani yake hutumiwa kwa kawaida kulisha mbuzi na ni chanzo kizuri cha protini na nguvu. BBC.



# Kwa kauli hii tata, Lema ahojiwe, achanguzwe

**Na Hamid Yassin**




MARA baada ya kutangazwa kwamba Paul Makonda ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema aliibuka na kauli kadhaa tata juu ya uteuzi huo.

Katika kauli alizitoa Lema ambaye alishakuwa Mbunge wa Arusha kwa vipindi viwili (2010 hadi 2020), ambayo imenistua mimi ni ile kwamba pamoja na Makonda kupata uteuzi huo lakini; "Kamwe hawezi kupata fursa ya kuua tena watu!"

Alaa! Kumbe Makonda ameshawahi kuua na akaachwa bila kufikishwa kwenye vyombo vya dola! Yaani Makonda yupo juu ya sheria za nchi hii na anaweza kufanya jambo baya kama hilo na akina Lema wakajua lakini hakuburuzwa mahakamani kama wauaji wengine wanavyoshughulikiwa!

Kutoa madai makubwa namna hiyo inatakiwa uwe na ushahidi vinginevyo uwe na kichwa kama cha mwenda wazimu hivi!

Madai ya kukurupuka kama haya ndio ndio wengine wakifikishwa mahakamani na kushindwa kuthibitisha madai yao huishia kudai kwamba wananyaswa kisiasa.

Pamoja na kuamua kuandika makala haya lakini siyo siri mshangao mkubwa umenigubika, hivi kwa nini Makonda mwenyewe yupo kimya juu ya kauli hizi nzito za Lema dhidi yake? Labda wanasiasa wamezoeana katika kauli kama hizi, hivyo amepuuza; Je, vyombo vya dola kwa nini navyo viko kimya?

Maana hapa hachafuliwi Makonda peke yake, hata vyombo vya dola vinachafuka, hivyo vilitakiwa kulifuatilia hili kwa kina aidha kwa kumkamata Makonda au huyu Lema anayetoa kauli hizi ili akazithibitishe mbele ya vyombo vya sheria.

Hata hivyo, nimedokezwa kwamba hiki ni kiwewe tu kimemkumba Lema baada ya Makonda kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha akihisi ametumwa akamdhibiti yeye asishinde Ubunge kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwakani ambao tayari ameshatangaza nia kwamba atajaribu tena bahati yake ya kurejea Bungeni kupitia jimbo la Arusha mjini.

Ni huo Ubunge tu unaomfanya Lema kumchafua mwenzake mitandaoni na habari za kuhusika na mauaji au wana ugomvi wao mwingine? Kama kweli ni ubunge basi ni hatari kubwa, Makonda aishi Arusha kwa tahadhari kubwa la sivyo yanaweza kumkuta ya kumkuta!

Tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi hapa nchini mwaka 1992, ukiondoa yale mauaji yaliyotokea Zanzibar mwaka 2001, mikoa miwili ya Kaskazini ya Kilimanjaro na Arusha ndio inaongoza kwa matukio ya mauaji na vurugu nyingi za kisiasa kuliko mikoa mingine yote hapa nchini.

Kule mitandaoni kulichafuka hasa baada ya Lema kuposti hiyo habari ya kwamba kamwe Makonda hawezi kupata fursa ya kuua tena watu, wengi wakimuuliza kiongozi huyo wa Chadema jinsi atakavyomdhibiti Mkuu huyo wa Mkoa wa Arusha 'asifanye tena hayo mauaji'!

Majibu yake yalikuwa mafupi kwa kila aliyemuuliza kwamba; "Kamwe hataua tena!"

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan akiongea kwenye hafla ya kuwaapisha wateule wake wiki iliyopita Jijini Dar es Salaam hakutamka kwamba amempeleka Makonda Arusha akamdhibiti Lema au kushughulika na masuala ya siasa tu, bali alitaja maeneo mengine kadhaa ambayo Mkuu huyo wa Mkoa anatakiwa akayasimamie.

Baadhi ya maagizo hayo ni pamoja na kwenda kusimamia utalii ambako alimweleza kwamba wageni ni wengi lakini malazi ni machache, pia akamtaka akasimamie masuala ya kimataifa kwani Arusha ni mji mkubwa ambao pia ni makao makuu ya Jumuiya Afrika Mashariki sambamba na taasisi nyingi za kimataifa zilizopo kule.

"Paul umekifanyia kazi nzuri chama, tumekupeleka Arusha unajua nini kipo kule na unajua matumaini yangu kwako, nenda kafanye kazi Arusha. Kubwa ni masuala ya utalii na Arusha ndiyo makao makuu ya Jumuiya ya Afrika mashariki na taasisi nyingine za kimataifa zipo pale, nenda kasimamie."

Hayo ndiyo yalikuwa maagizo ya Dk. Samia kwa Makonda, hakuna cha Lema hapo wala Chadema.

Hii si mara ya kwanza kwa Lema kuibuka na kauli tata na mara zote huwa ananusurika kupata adhabu kubwa. Mwishoni mwa mwaka jana alisakwa na vyombo vya dola kwa madai ya kumtishia maisha Mtendaji wa Kijiji cha Korongwe, Daud Ismail wilayani Nkasi Mkoa wa Rukwa.

Agizo la kukamatwa kwa Lema lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Mhe. Peter Lijualikali kwa maelezo kuwa, alitaka ahojiwe kwa kutoa kauli za uchochezi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Oktoba 24, 2023 katika kijiji hicho kilichopo kitongoji cha Forodhani, Kata ya Fipa.

"Namuagiza OCD wa Nkasi, kuchukua hatua za kisheria mara moja kumuita kokote aliko Godbless Lema ili afike Nkasi akafanyiwe mahojiano kuhusu kauli yake ya kichochezi ya kuhatarisha hali ya usalama ya mtendaji huyo katika eneo letu na kukwaza juhudi za wananchi kufanya shughuli za maendeleo," alikaririwa Lijualikali.

Hata hivyo, hadi leo hatima ya agizo lile haieleweki liliishia wapi.

Hivi pale Lema atasema alikuwa anaipigania Chadema ama anaihujumu? Wananchi gani wenye akili timamu wanaweza kumuunga mkono yeye mwenyewe ama chama chake kwa kauli kama zile za kiwendawazimu za kumtishia maisha na kumdhalilisha Mtendaji yule wa Kijiji?

Umefika wakati viongozi hawa wa kisiasa wawe wanapimwa akili zao ijulikane iwapo wako timilifu vichwani mwao ama la, kama ilivyowahi kupendekezwa kule Bungeni miaka kadhaa iliyopita!

Hata tukio la kule Korongwe Nkasi Mkoa wa Rukwa si mara ya kwanza kwa Lema kutoa hizi kauli zake tata na za udhalilishaji kwa viongozi na watendaji mbalimbali wa taifa hili.

Wakati fulani akiwa Mbunge wa Arusha mjini aliwahi kutoa kauli ambazo hata mtoto wa darasa la kwanza hawezi kuongea akiwa ndani ya chombo kikubwa cha kutunga sheria, yaani ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini yeye alifanya hivyo!

Kwa wale wanaokumbuka kama mimi, nadhani bado wanazikumbuka zile klipu zilizosambaa mitandaoni zikimwonyesha huyu Lema akimtabiria kifo aliyekuwa kiongozi mmoja wa juu wa taifa hili!

Kwamba angefariki dunia kabla ya mwaka 2020! "Utabiri' ule alioutoa Lema Bungeni ndiyo ulikuwa mwanzo wa baadhi ya Wabunge kutaka kuwe na utaratibu wa kuwapima akili ili kuwabaini wale wanaotumia bangi na dawa za kulevya.

Mimi niliwaunga mkono kwa asilimia mia wabunge wale, kwani kwankauli ile ya Lema ni ukweli usiopingika kuwa maneno yale aliyasema akiwa hayuko sawa kichwani! Bila kufanya vile Bunge letu lingekosa maana. Vitu vya kujiuliza hapa Watanzania wenzangu na kutafakari kwa kina hivi hii jeuri ya kutoa kauli tata mara kwa mara Lema anaitoa wapi?

Kitu gani huwa kinamsukuma mpaka kujiamini mpaka kutoa matamko kama hayo? Je, kuna watu nyuma yake wanaomlinda? Kama wapo akina nani hao?

Maana katika lile sakata la kule Korongwe Nkasi, Lema alijibu kwa jeuri kwamba yuko kijiweni Arusha anasubiri hivyo vyombo vya dola vikamkamate!

Huyu ni mtu aliyerudi nchini Machi mwaka jana baada ya kukimbia nchi tangu mwaka 2020 na kimsingi alikimbia tu kivuli chake mwenyewe. Hivi hii haiwezekani kwamba anaweka mtego kwa Serikali wamswekwe 'lupango' ili ionekane Tanzania haina utawala wa kisheria?

Huyu alihifadhiwa Canada kwa miaka karibu miwili, nchi ambayo kwa kushirikiana na baadhi ya vyama vya kihafidhina vya Ujerumani ndiyo wafadhili wakuu wa chama chao cha Chadema!

Kwa kuwa wanakula fedha zao na kupokea misaada yao mbalimbali hutaka kuwaonyesha eti nao wanapambana huku! Kumbe ni maigizo matupu na uvunjifu wa sheria za nchi!

Wana kawaida ya kuanzisha tafrani na wanapodhibitiwa na vyombo vya dola hurekodi matukio hayo na kutuma 'klipu' huko kwa wahisani wao kuonesha eti huwa wanapambana kutaka kushika dola lakini huhujumiwa!

Kauli hii ya Lema kwamba Makonda ni muuaji ni tuhuma nzito na udhalilishaji mkubwa uliofanywa na kiongozi huyo wa Chadema ambao ungefanywa na viongozi wa Serikali ama CCM sasa hivi ungesikia kelele nyingi ndani na nje ya nchi.

Kauli hii ingekuwa imetamkwa na kiongozi wa chama tawala dhidi ya wale wa upinzani, zile taasisi za haki za binadamu zingekaa kimya?

Je, viongozi wa vyama vya upinzani wangekaa kimya na kuona ni jambo la kawaida kama ilivyo sasa?

Lema aache kuweweseka. Jimbo la Arusha si mali yake ndiyo maana hivi sasa lipo chini ya mikono salama ya CCM kupitia Mbunge wake, Mrisho Gambo. Kama analitaka aache kuchafua watu, asubiri wakati ufike aingie kilingeni!

***Kwa maoni au ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020***



# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462



# Serikali inawekeza vyema kwenye afya, kazi ni kwenu watendaji

SEKTA ya afya ni miongoni kwa sekta muhimu katika nchi kwani ina mchango mkubwa katika kuwezesha wananchi kutimiza majukumu yao ya kila siku likiwemo jukumu kubwa la ujenzi wa taifa.

Ili wananchi waweze kutimiza kikamilifu jukumu la ujenzi wa taifa lao kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi wanazozifanya, mathalani, shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji, viwanda, biashara, ujasiriamali na kadhalika, ni lazima wananchi wawe na afya njema, ndiyo maana Wizara ya Afya ina msemo usemao "Mtu ni Afya, Jali Afya Yako."

Mtu anapokosa afya njema, hawezi kuzalisha, atatumia fedha nyingi kujitibu lakini pia ndugu wanaomzunguka watalazimika kuacha shughuli za uzalishaji ili kumuuguza.

Kutokana na umuhimu na unyeti wa kipekee wa sekta ya afya, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi shupavu wa Dk. Samia Suluhu Hassan, sekta hii imepatiwa kiasi cha shilingi Trilioni 6.722 kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya katika ngazi zote ili wananchi popote walipo wanufaike na huduma za afya.

Akizungumza na waandishi wa habari kuelezea mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia katika sekta ya afya, Waziri Ummy Mwalimu anasema: "Ndani kipindi cha miaka mitatu serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya, upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini, kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa ikiwemo huduma za mionzi, kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, kudhibiti maambukizi ya HIV/UKIMWI, kifua kikuu, malaria na magonjwa ya mlipuko, ajira kwa watumishi na ufadhili wa wanafunzi katika ngazi za fani mbalimbali pamoja na kupitishwa kwa sheria ya bima ya afya kwa wote."

Ikumbukwe kuwa miongoni mwa vipaumbele sita vya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni pamoja na ubora wa huduma za afya inayotolewa kwa wananchi. Wizara imeweka mkazo na msukumo mkubwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kwani pamoja na uboreshaji na ujenzi wa miundombinu bora ya afya iliyopo sasa, kama wananchi hawatapewa huduma bora, miundombinu hiyo haitakuwa na maana kwa wananchi wanaohitaji huduma.

Akizungumza na Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Afya Aprili 4, 2024 lililokutana kwa siku moja jijini Dodoma kwa ajili ya kupitia utekelezaji na ufafanuzi wa hoja mbalimbali pamoja na mikakati ya kutoa huduma bora kwa wananchi sambamba na kujadili bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025, Waziri Ummy Mwalimu alisisitiza wahudumu wa wizara ya afya kuzingatia ubora wa huduma za afya wanazozitoa kwa wananchi kwani ubora wa huduma zao ni agenda muhimu katika wizara hiyo.

Waziri Ummy alisisitiza kuwa serikali inafanya juhudi kubwa kufikisha huduma bora wa kwa wananchi popote walipo. "Tunajua tumefanya vizuri sana kwenye miundombinu na vifaa tiba, lakini tumeendelea kulalamikiwa kwenye eneo la huduma, hususani ngazi ya msingi, huku juu kwenye kanda na ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa, tumejitahidi sana.

"Rai yangu kwenu tuendelee kusaidia katika kuimarisha huduma kwenye zahanati, hospitali za wilaya na vituo vya afya. Jambo tukishakubaliana kwenye vikao halali, tunatakiwa kwenda kwenye utekelezaji, tunapoendelea kuzunguka na kupiga danadana tunawakwamisha wananchi na mwisho wa siku tunalaumiwa. Niliombe baraza hili, mnapojadiliana suala hili mlipe kipaumbele." amesema Waziri Ummy.

Kimsingi, haipendezi uwekezaji mkubwa uliofanyika katika sekta ya afya ukachafuliwa kwa wananchi kuendelea kulalamikia huduma zinazotolewa na wahudumu wa afya hasa katika matumizi ya lugha na kujali muda katika kuwahudumia wananchi.

Pindi mwananchi anapofika kwenye kituo cha kutolea huduma anahitaji kupata faraja kutoka kwa watoa huduma kupitia lugha nzuri, ya staha na ya upole. Huduma bora kwa wateja pekee inaweza kumpa mgonjwa unafuu katika ugonjwa unaomsumbua. Hivyo basi, ni vyema wananchi wakapokelewa, kusikilizwa, kuhudumiwa na kupata huduma zote muhimu ili mwananchi aone umuhimu wa kwenda kupata huduma za afya kwenye vituo rasmi.

Februari 15, 2024, akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kisera wa 23 wa Sekta ya Afya uliofanyika jijini Dodoma, Waziri Ummy alisema: "Suala la ubora wa huduma za afya tunaendelea kulisisitiza kwa kuzingatia umuhimu wa kuboresha huduma kwa wateja pamoja na kuhakikisha usalama wao ili mteja apate huduma iliyokuwa nzuri."

Kwahiyo, kitendo cha Waziri Ummy kuendelea kusisitiza utoaji wa huduma bora kwa wananchi mara kwa mara kila apatapo nafasi ya kuzungumza, kinaonesha ni kwa namna gani amedhamiria kuona wananchi wanapata huduma bora kwani sekta ya afya inawahudumia wananchi moja kwa moja, uso kwa uso kila siku katika ngazi mbalimbali kuanzia kwenye vijijini hadi mijini.

Kama hiyo haitoshi, akiwa mkoani Shinyanga mwezi Julai, 2023 kwenye ziara ya kikazi, Waziri Ummy aliwasisitiza wataalamu wa afya kuboresha zaidi utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia matumizi ya lugha na kauli zenye staha kwa wananchi na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vipimo ili kuwawezesha wananchi kupata huduma bora za afya.

Waziri Ummy alisema: "Ndugu zangu wataalamu wa afya, nipende kuwasisitiza sana katika kuzingatia weledi, maadili, miiko na utu katika utoaji wa huduma kwa wananchi wetu huku tukitumia muda mwingi zaidi kutatua kero na kupunguza malalamiko kwa wananchi wetu na kwa kuhakikisha pia madaktari mnaandika dawa kwa kufuata miongozo ya vitabu vya dawa vya taifa ili kuondoa malalamiko kwa wagonjwa wetu."

Pengine sasa ni wakati mwafaka kwa wahudumu, watumishi na wataalamu wa afya kubadilika na kuhakikisha wananchi wanaofika kupata huduma wanawahudumia vizuri.

Sekta ya afya imebeba uhai wa binadamu, hivyo ni muhimu kuwahudumiwa wananchi vizuri ili waweze kupona na hatimaye kurejea kwenye shughuli zao za uzalishajimali kwa kuwa na afya njema kwa maendeleo yao na ya taifa pia.

Kwangu mimi, sina deni kwa Waziri mwenye dhamana ya afya-Ummy Mwalimu kwani amesisitiza vya kutosha uzingatiaji wa utoaji wa huduma bora za afya kwa wagonjwa, kazi kwenu wataalamu wa afya kutendea kazi maagizo na maelekezo haya. Tafakari, chukua hatua.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

# TABIA UNAZOTAKIWA KUZIACHA HARAKA ILI KUSONGA MBELE

**1. ACHA KUPENDA KUWARIDHISHA AU KUWAFURAHISHA WATU.**

Hili ni tatizo kubwa kwa jamii yetu hususan jamii za kijamaa ambazo watu wanaishi kama ndugu. Watu wanapenda maoni ya watu na wanajaribu kumfanya kila mmoja aridhike. Tabia hii itakufanya ujitahidi kufanya wanavyotaka watu na mwisho kujikuta uko kama wao.

Tabia hii inakuondolea upekee wako (Uniqueness) ambayo ni moja ya siri kubwa za kufanikiwa. Ukitaka kusonga mbele, hakikisha wazo lako, lipime kwa vipimo sahihi (smart) kisha jiamini na usonge mbele (Be yourself).

**2. ACHA KUJILINGANISHA NA WENGINE (NEVER COMPARE YOURSELVES WITH OTHERS).**

Kwenye maisha unahitaji kufanya tofauti ili kupata matokeo tofauti. Ukitaka kujilinganisha na wengine tegemea matokeo waliyoyapata.

**3. ACHA KUJISHTUKIA –**

Ukiamua kufanya jambo, anza hatua za kufanya, acha kujistukia na kujiona kama huwezi. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa wazo lako ni sahihi. Hakuna siku utajiona unaweza, unachotakiwa ni kuanza kisha katika safari unajenga uwezo. Wote wanaofanya makubwa, kuna siku waliamua na kuanza na ukiwauliza, watakwambia kuwa uwezo wao umeendelea kujengeka siku baada ya siku. Acha kujishtukia na kusitasita. Ukiamua anza na usonge mbele.

**4. ACHA KUKIMBIA CHANGAMOTO**

Vikwazo ni sehemu ya safari. Tafuta jinsi ya kutatua na si kukimbia. Hakuna kisicho na changamoto. Hata ukiamua kulala siku mbili utapata changamoto tu ya kuumwa mbavu. Usikimbie changamoto kabiliana nazo kwa kutafuta njia na kuzitatua.

**5. ACHA KUJIDANGANYA/ KUJIRIDHISHA**

Mara zote Tafuta uhalisia ili ukupe njia sahihi. Usichukulie mambo kirahisi. Hakiki njia zako bila kudharau wala kuchukulia poa. Kwa lugha rahisi hapa nasisitiza uwe makini na ufanye mambo kwa tahadhari na kumaanisha hata kama unachofanya ni kidogo.

**6. ACHA KUFANYA KAWAIDA (ILI MRADI)**

Mara zote fanya kwa ubunifu, maarifa na ustadi. Tambua chochote kisichokuuma hakitawagusa wengine. Ukifanya mambo kiholela matokeo yake ni holela pia. Unapofanya jambo, tuliza akili, kuwa mbunifu, jiulize maswali mengi, wekeza nguvu ili upate kilicho bora.

**7. KUTOFANYA MAANDALIZI YA KINA**

Jiandae vizuri kwa kila kilicho mbele



yako. Maandalizi mazuri yanakupa urahisi na manufaa makubwa kwenye kulifanya jambo. Mfano mchezo wa dakika 90 wa mpira, unaweza kuandaliwa mwezi mzima. Mchezo wa ngumi wa round nane, unaandaliwa miezi mitatu au zaidi. Hapa nakuonesha umuhimu wa kujiandaa na kitu unachokifanya.

**8. ACHA VISINGIZIO**

"Ukihitaji jambo utatafuta njia, lakini kama hutaki utatafuta visingizio". Hakuna kushindwa kunakokosa visingizio.

Ukitaka kufanikiwa, acha kutafuta visingizio (excuses). Kiri kushindwa na uangalie nini kilikufanya ushindwe kisha amua kuwa hutashindwa tena.

**9. ACHA UBINAFSI**

Njia yako inahitaji watu sahihi ambao una nafasi kwao nao wana nafasi kwako. Watu wanaweza kuwa sababu ya uimara wako au sababu ya anguko lako. Pamoja na angalizo hilo bado ukweli ni kwamba unahitaji watu ili kusonga mbele.

Unachotakiwa kufanya ni mambo mawili makubwa, acha ubinafsi na uchague watu sahihi.

**10. ACHA KULALAMIKA SANA**

Tabia hiyo inakufanya ujioneshe dhaifu usiye na uwezo wa kubadili hali ila unataka huruma za watu.

(You sound Powerless) Monitor your behavior.

**11. ACHA KUKOSOA KILA KITU**

Jifunze kuona mema zaidi kuliko mabaya (Positive Mindset). Huwezi kupata kitu usichokiona mara kwa mara. Ukiwa kila wakati unaona ubaya na kukosoa, hatuwezi kutegemea matokeo mema kwako. Badili mtazamo, kulalamika sana ni zao la mtazamo hasi.

**12. ACHA TABIA YA KUAHIRISHA MAMBO (PROCRASTINATION).**

Tabia hii inaweza kuwa moja kati ya tabia chache kubwa zinazowafanya wengi kutopiga hatua. Jiulize unapanga mambo mangapi na unatekeleza mangapi? Utagundua hata wewe ni mhanga na mwathirika wa ugonjwa huu mkubwa wa kuahirisha mambo.

**13. KUTAKA KUWA SAHIHI WAKATI WOTE (PERFECTIONISM)**

Ni muhimu sana kuhakikisha kuwa unakuwa sahihi, lakini kuacha kufanya mambo kwa ajili ya kutafuta usahihi tu kutakuchelewesha sana.

**14. ACHA TABIA YA KUSEMA "NDIYO" HATA MAHALI AMBAPO ULITAKIWA KUSEMA "HAPANA"**

Watu wengi tunadhani kusema ndiyo ni unyenyekevu au busara. Jambo la kwanza ni vizuri kila siku

uwe na ratiba ya mambo ya kufanya (To do list). Kama wewe una ratiba yako ya mambo ya kufanya, halafu kikija kitu kingine hutakubali kila kitu ili kutekeleza ratiba yako. Ndiyo yako iwe ndiyo kama una nafasi na kama huwezi au huna nafasi, sema hapana.

**15. ACHA MAWAZO (MTAZAMO) HASI YAANI KUONA KUSHINDWA TU**

- Negative Perception. Ni vizuri kuwa na muda kujiuliza wewe Unaona nini kwenye maisha. Huwezi kupata matokeo usiyoyaona kwenye mtazamo kwanza. Kama kuna vitu vya kuviacha kwa haraka ni mtazamo hasi.

**16. ACHA KUPUUZA MALENGO YAKO NA KUTOKA KWENYE NJIA**

(Lack of self Determination).

Siku zote timiza malengo usitoke kwenye lengo lako wala kuacha njia yako.

**17. ACHA KUWA NA MTAZAMO WA PESA KULIKO MATOKEO YA KULETA SULUHU YA TATIZO KWENYE JAMII.**

Wazo lako ni vizuri ukilipanga kwa kuangalia matokeo yake chanya kwenye kuwahudumia watu au kutatua tatizo fulani kwenye jamii. Wazo lolote linalolenga kutatua tatizo kwenye jamii litanunuliwa kwa gharama yoyote. Lakini mpango ukilenga fedha, inaweza kukusumbua.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa Taasisi, Kikundi, Kanisa, Umoja, NGO au mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu. Karibu uwasiliane nasi kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com

***We work Consult***
***Your Partner in Growth.***

# Mwani unavyoimarisha uchumi wa wanawake Z'bar

**Na Muznat Haji**

TOFAUTI na aina nyingine ya kilimo ambapo mkulima hulazimika kuchimba ardhi kwa kutumia jembe ama zana nyingine, kuweka mbegu akitarajia mmea kuota ardhini, kilimo cha mwani ni tofauti. Zao hili hulimwa kwenye maji ya bahari.

Kwa Zanzibar, historia inaonesha kwamba, kilimo cha mwani kilianza mwishoni mwa mwaka miaka ya 1980. Kuanzishwa kwa kilimo hiki ni kama kileleta mgawanyo wa kazi linapokuja suala la uchumi wa buluu baina ya wanawake na wanaume ambapo wanaume wameendelea kufanya kazi za uvuvi huku wanawake wakiingia kwenye kilimo hicho cha mwani.

Awali, wanawake wengi waliokuwa wakijishughulisha na kilimo cha mwani ni wale waliokuwa kwenye mazingira magumu kama vile wajane. Hawa ndio waliojitosa kwenye kilimo hiki wakikiona kama mkombozi wao.

Kutokana na faida za kiuchumi na kuongezeka umaarufu wa kilimo cha mwani, wanawake wengi wameingia kwenye kilimo hiki na kwa sasa ni sahihi kusema kwamba zao la mwani limekuwa moja ya nguzo ya kiuchumi kwa akina mama wengi Zanzibar.

Mwani unaweza kuuzungumzia kuhusu ubora wa bidhaa zake kama kirutubisho mwilini, sabuni, jam, mafuta na kadhalika, lakini leo makala haya yanalenga kuangalia, japo kwa ufupi, namna zao hili linavyowanufaisha kiuchumi akina mama na kubadilisha maisha yao.

### KUBOREHA MAISHA YA WANAWAKE

Mariyam Mussa Haji, mkazi wa Fuoni Melitano, ambaye ni mwanzilishi wa kikundi cha Muzne Products chenye watu watatu, anasema thamani ya zao la mwani imeongezeka ikilinganishwa na miaka iliyopita.

"Thamani ya zao la mwani imeongezeka kwa sababu sehemu ya mwani inayozalishwa hapa Zanzibar inasarifiwa na kuzalisha bidhaa mbalimbali (zilizoongezwa thamani)," anasema Mariyam.

Anasema tofauti na zamani ambapo mwani wote uliozalishwa Zanzibar ulisafirishwa nje, hivi sasa hatua ya mwani kuzalishwa bidhaa hapa nchini kumeongeza mnyororo wa thamani kwa wajasirimali, hasa wanawake.

Mariyam anazidi kusema kwamba tangu kikundi chao kianze kuuza bidhaa zitokanazo na mwani, wamekuwa wakipata faida kubwa na hivyo kujikwamua kimaisha kutokana uuzaji wa bidhaa hizo.

Miongoni mwa bidhaa zinazozalishwa na Muzne Products, kikundi kilichopo Fuoni Meli Tano ambazo mwandishi wa makala haya amebatika kuziona ni pamoja na sabuni, mafuta, jam na unga wa lishe wa mwani.

"Kwa kiasi fulani fedha tunazopata zinatusaidia kimarisha na kuepukana na ukali wa umasikini. Wengine wamepata ajira za kudumu kwa kuuza bidhaa hizi tunazozalisha," anasema Mariyam.

Anasema kwa mwezi mmoja, kutegemea sana hali ya soko, wana uhakika wa kuingiza kuanzia shilingi 300,000 na kundelea.

"Kwa kawaida biashara inaenda na msimu kwa wastani tunaweza kuingiza Sh. 500,000 pale biashara inapokuwa nzuri lakini haikwenda vyema hatukosi shilingi 300,000. Alhamdulillahi," anasema.

Mariyam anasema wanunuzi wakubwa wa bidhaa za mwani mara nyingi hutoka Tanzania Bara pamoja na wazungu wanaotembelea katika maduka yao.

Kwa upande wake, Mwanaisha Makame ambaye ni mmoja ya wachakataji wa zao la mwani kutoka Paje, anasema kazi hiyo imesaidia kumwinua kiuchumi kwani amefanikiwa kuwasomesha watoto wake wawili katika ngazi mbalimbali.

Safia Hashim mkaazi wa Muungoni, Wilaya ya Kusini Unguja, anasema yeye ni mmoja kati ya wanawake wanaofaidika na kilimo cha mwani, ambapo amefikia hatua ya kumiliki nyumba.

Safia anasema alipata mafunzo ya miezi mitatu kutoka kwa mtaalamu kutoka Indonesia ambayo yamemwezesha kuwa na ujuzi wa kusarifu zao la mwani.

"Kwa sasa naweza kutumia mwani kutengeneza vitu mbalimbali kama vyakula, juisi, chachandu, pilipili, kachumbali, chipsi, tambi, chauro, visheti, keki, pipi, jam ya matunda, sabuni, shampoo na mafuta ya kupaka na ya nywele," anasema Safia.

Joyce Denis, Ofisa Uvuvi, Kitengo cha Mwani katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, anasema hatua ya wajasirimali kuzalisha bidhaa mbalimbali kumeliongezea thamani zao hilo la mwani.

Ofisa huyo anabainisha kuwa bidhaa zinazotokana na mwani zinasaidia wanawake wajasirimali kuongeza mapato na kuchochea bei katika soko ikilinganishwa na mwani mbichi.

Aidha anasema bidhaa zitokanazo na mwani husaidia kuimarisha afya ya jamii, kutokana na ukweli kwamba bidhaa zitokanazo na zao hilo zinaposarifiwa na kuwa chakula husaidia mwili wa mwanadamu kupata virutubisho muhimu.

### KUTOKA MALIGHAFI HADI BIDHAA

Kilimo cha mwani kimewapatia ajira za kudumu wanawake wengi katika sehemu za pwani za vijiji vya Zanzibar, ambapo baadhi ya akina mama waliozungumza na mwandishi wa makala haya wamesema pamoja na kwamba kilimo hicho ni kigumu lakini kimebadilisha maisha yao.

Wanawake wengi wamejiajiri katika kilimo hicho, ingawa wengi wao wanasema kuwa licha ya kazi kubwa, bado kipato ni kidogo lakini si sawa na kuka bure.

Hata hivyo, anasema tofauti na zamani ambapo mwani uliuzwa ukiwa ghafi, sasa wanazalisha bidhaa nyingi kutokana na zao hilo na hivyo kuongeza thamani tofauti na kuuza mwani ghafi.

### ONGEZEKO LA UZALISHAJI

Kwa mujibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, uzalishaji wa zao hilovisiwani umeongezeka kutoka, tani 10,531 kwa mwaka 2021, hadi tani 12,594 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 20.

Kwa mujibu wa taarifa za wizara hiyo, usafirishaji wa mwani nje ya nchi umeongezeka kutoka tani 12,124 kwa mwaka 2021 hadi tani 13,972 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.

Zanzibar ni nchi ya nne 4 duniani kati ya nchi zinazozalisha mwani mwekundu, ikiwa nyuma ya nchi ya Indonesia, Ufilipino na Malaysia, ambapo mwaka 2021 Zanzibar ilizalisha zaidi ya tani 12,000. Hata hivyo, juhudi zikizidi kufanyika, upo uwezekano wa kuzipuku baadhi ya nchi.

### AWAMU YA NANE NA KILIMO CHA MWANI

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anasema Zanzibar ni nchi inayoongoza kwa uzalishaji wa mwani barani Afrika na umekuwa ukiongezeka.

Anasema ili kupata mafanikio zaidi ndio maana serikali imeunda sera mpya ya uchumi wa buluu pamoja na mikakati ya uzalishaji wa mazao ya baharini ukiwemo mwani.

Rais anasema serikali imewekeza fedha nyingi katika kuwasaidia wakulima na wajasiriamali wa sekta ya mwani wapatao 5,000 Unguja na Pemba kwa kuwapatia boti maalumu za kuwawezesha kwenda katika maji ya kina kirefu zaidi kwa ajili ya ulimaji wa mbegu bora za mwani.

### TAFITI ZA KITAALAMU

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Suleyum Talib Ali kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ulioangazia mchango wa kilimo cha mwani katika uchumi wa buluu, ulieleza kuwa zao hilo limekuwa na nafasi ya pekee katika kusaidia maisha ya wakulima.

Kwa mujibu wa utafiti huo, mkulima wa mwani kwa mwezi ana uhakika wa kupata kati ya shilingi 120,000 hadi 200,000, ambazo humsaidia katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaisha katika familia.

Mtafiti mwingie wa mwani, Flower Msuya, yeye anasema kilimo cha mwani kinasaidia kwa kiasi kikubwa maisha ya wakulima na wajasirimali wanaouza bidhaa za zao hilo.

Anasema mwani ni wa pili kuingiza fedha za kigeni Zanzibar na kwamba kilimo cha zao hilo kina manufaa makubwa sana kwa wanawake wa visiwa hivyo kwa kuwa kimeboresha maisha yao.

"Katika utafiti wetu tumebaini kuwa mwani unaoitwa cottonie unaweza kulimwa kwenye maji mengi na ndio mwani bora zaidi, hivyo tunatumia tuber note kulima mwani huo. Njia hiyo inatumia neti na bomba kupanda mwani kwenye bahari badala ya vijiti," anasema.

DIRA YA MAENDELEO Z'BAR

Kwa kutambua shughuli za wakulima wa mwani, Dira ya Mpango wa Maendeleo-endelevu ya Zanzibar ya mwaka 2020-2050 imeeleza kwamba kupitia matumizi sahihi ya bahari chini ya mikakati ya mwelekeo wa uchumi wa buluu ni kupatikana faida ya ajira na kupunguza umasikini kwa watumiaji wa rasilimali hiyo.

Aidha dira imeuweka uchumi wa buluu kama sekta muhimu ya kiuchumi ambayo itaufanya uchumi wa Zanzibar kuwa endelevu.

Dira hiyo inakwenda sambamba na malengo ya 14 na 6 ya agaenda ya Bara la Afrika 2063, ambayo inasisitiza matumizi mazuri na endelevu ya bahari katika kuleta maendeleo.



# Hatma ya Zuma kugombea au la mikononi mwa Majaji

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

MAJAJI nchini Afrika Kusini, jana Jumanne, walitarajiwa kuamua ikiwa Rais wa zamani, Jacob Zuma, ataruhusiwa kugombea kwenye uchaguzi wa Mei, mwaka huu.

Zuma, ambaye anawania kupitia chama cha upinzani, alikata rufaa dhidi ya uamuzi wa maafisa wa Tume ya Uchaguzi waliomkatalia kugombea kutokana na kupatikana na hatia mwaka 2021.

Juzi Jumatatu, Zuma (81), alikuwa mahakamani mjini Johannesburg wakati mawakili wakijadili kesi hiyo.

"Ikiwa raia wanataka niwe Rais, nani atawazuia?," Zuma aliwambia wafuasi wake baada ya kesi kusikilizwa, " alisema Zuma na kuongeza: "Niruhusu niende na nimalizie kile nilichokianza."

Afrika Kusini inafanya uchaguzi mkuu Mei 29, mwaka huu ambao unatarajiwa kuwa uchaguzi wenye ushindani mkali tangu ujio wa demokrasia mwaka 1994.

Kwa sasa, Serikali ya Afrika Kusini inatawaliwa na Chama cha African National Congress (ANC). VOA.



Rais wa zamani, Jacob Zuma

# Israel yaonywa kutoishambulia Rafah



**CAIRO, Misri**

VIONGOZI wa Misri, Ufaransa na Jordan, wameionya Israel kuwa mashambulizi dhidi ya mji wa Kusini wa Gaza wa Rafah yatakuwa na matokeo hatari.

Walisema kwa pamoja kwamba italeta tu vifo na mateso zaidi na kutishia kuongezeka kwa vita katika kanda hiyo.

Marekani pia ilisema inapinga mashambulizi yoyote dhidi ya Rafah, ambapo zaidi ya Wapalestina milioni 1.5 wanajihifadhi.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema tarehe ya shambulizi hilo sasa imepangwa, lakini hakutoa maelezo yoyote.

"Leo nimepokea ripoti ya kina kuhusu mazungumzo ya Cairo, tunajitahidi mara kwa mara ili kufikia malengo yetu, kwanza kabisa kuachiliwa kwa mateka wetu wote na kupata ushindi kamili dhidi ya Hamas," alisema juzi Jumatatu na kuongeza:

"Ushindi huu unahitaji kuingia Rafah na kumaliza ugaidi huko. Itafanyika tarehe imepagwa."

Wakati huo huo, Waziri wa Ulinzi wa Israe, Yoav Gallant, amependekeza kwamba sasa ulikuwa wakati mwafaka wa makubaliano juu ya mateka, miezi sita ikiwa vitani na Hamas.

Maoni hayo yanatolewa wakati mazungumzo ya kubadilishana wafungwa na kusitisha mapigano, yakiendelea katika Mji Mkuu wa Misri - Cairo. BBC.

# Jaji apinga ombi la Donald Trump

**NEW YORK, Marekani**

JAJI mmoja wa Mahakama ya Rufaa ya New York, amepinga ombi la Rais wa zamani, Donald Trump, la kuchelewesha kesi yake ya jinai ya Aprili 15, wakati akipambana kuondoa kesi hiyo kutoka mji wa Manhattan, huko New York.

Uamuzi huo ulitolewa juzi Jumatatu, wiki moja kabla ya uteuzi wa jopo la mahakama kuanza.

Mawakili wa Trump walikuwa wamewasilisha hoja katika kikao cha dharura, wakidai kwamba kesi hiyo ya kihistoria, inapaswa kuahirishwa, wakati wakitetea haja ya kuihamisha kutoka mji wa Manhattan wenye wafuasi wengi wa chama cha Democratic.

Trump amependekeza kupitia jumbe za mitandao ya kijamii kwamba, kesi hiyo ihamishiwe Staten Island, Jimbo pekee la New York ambalo alishinda katika uchaguzi wa mwaka 2016 na ule wa 2020.



Rais wa zamani, Donald Trump

> "Mawakili wa Trump walikuwa wamewasilisha hoja katika kikao cha dharura, wakidai kwamba kesi hiyo ya kihistoria, inapaswa kuahirishwa, wakati wakitetea haja ya kuihamisha kutoka mji wa Manhattan wenye wafuasi wengi wa chama cha Democratic.

## "...tarehe ya kuushambulia mji wa Rafah imepangwa"

**GAZA, Israel**

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amesema tarehe ya mashambulizi ya ardhini, yakilenga mji wa Ksini mwa Gaza wa Rafah, imepangwa, lakini bila kutaja ni lini.


Hayo yalijiri huku White House ikisema wapatanishi wake mjini Cairo, walikuwa wamewasilisha kwa wanamgambo wa Hamas, pendekezo la mpango wa kusitisha mapigano na kuachiliwa kwa mateka.

"Leo, nilipokea ripoti ya kina kuhusu mazungumzo ya Cairo," Kiongozi huyo wa Israel alisema huko Yerusalem na kuongeza:

"Tunajitahidi sana ili kufikia malengo yetu, kwanza kabisa kuachiliwa kwa mateka wetu wote, na kupata ushindi kamili dhidi ya Hamas. Ushindi huu unajumuisha kuingia Rafah na kutokomeza vikosi vya kigaidi vilivyoko huko. Tarehe imepangwa," alisema Netanyahu.

Mara moja Marekani ilimkemea kiongozi huyo wa Israel kufuatia kauli hiyo. Msemaji wa Wizara ya Ulinzi alisema "Tumeweka wazi msimamo wetu kabisa kwamba hatuungi mkono operesheni za Rafah."

"Tunataka kuona mpango wa kuaminika wa jinsi watakavyoendesha shughuli zozote huko" kutokana na wasiwasi mkubwa wa kibinadamu, kuhusu zaidi ya raia milioni moja wa Kipalestina walio huko, alisema naibu msemaji wa Pentagon Sabrina Singh.




Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu

# Makocha weusi ngumu kuajiriwa Ulaya

## ● Vincent Kompany na Nuno Espírito Santo, ndiyo Mameneja pekee weusi England



Vincent Kompany



Nuno Espírito Santo

**LONDON, England**

WACHEZAJI wasio weusi wana uwezekano wa hadi asilimia 50 kupata ukocha katika timu kuliko wachezaji weusi katika kipindi cha miaka 30, kulingana na utafiti wa taasisi ya Black Footballers Partnership (BFP) ya Uingereza.

Ripoti ya wasomi watatu iliangalia maisha ya nje ya uwanja ya takribani wanasoka 3,500 wa zamani waliocheza Ligi Kuu ya Uingereza au Klabu Bingwa kati ya 1990 na 2010.

Iligundua licha ya wachezaji weusi kuwa na asilimia 25 ya sifa za ukocha zilizotolewa na Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), miaka ya 2022 na 2023, walichangia asilimia 4 pekee ya majukumu ya ukocha.

Delroy Corinaldi, Mkurugenzi Mtendaji wa BFP, anasema; "Kazi katikausimamizi wa soka mara nyingi inaonekana ni kazi inayoongeza watu, lakini kwa wachezaji wa zamani weusi, hawaongezeki katika kazi hiyo"

BFP ni Shirika la Wachezaji weusi waliopo na wa zamani.

Ripoti hiyo ilitoa muhtasari kwamba wachezaji wa zamani weusi hupata nafasi chache kwenye usimamizi, hupandishwa vyeo polepole zaidi, maendeleo yao hukwama haraka na hufukuzwa kazi haraka kuliko wenzao wasio weusi.

Pia ripoti hiyo ilieleza mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na kocha mweusi ana uwezekano wa asilimia 41 kufutwa kazi kuliko kocha mzungu, wakati vipengele kama vile utendakazi ni sawa. Na katika majukumu yote ya usimamizi, mtu mweusi ana uwezekano wa asilimia 17 kufutwa kazi.

Kati ya wachezaji 3,500 katika utafiti huo, asilimia 73 ya wachezaji weusi walicheza Ligi Kuu ya Uingereza kwa wastani wa mechi 62 kwa kila mchezaji, huku asilimia 62 ya wachezaji wasio weusi walionekana kwenye ligi kuu, na wastani wa mechi 49.

"Matokeo ni ya kushangaza sana," Corinaldi aliambia Shirika la Habari la PA.

"Wachezaji kandanda wamekuwa kizazi kilichopotea nje ya uwanja, licha ya kuwa walikuwa nyota ndani ya uwanja."

Ripoti hiyo ilichapishwa muda mfupi baada ya kuthibitishwa kuwa serikali ya Uingereza itaanzisha msimamizi huru wa soka wakati Mswada wa Utawala wa Soka utakapowasilishwa Bungeni siku ya Jumanne.

Wachezaji wa zamani wakiwemo Les Ferdinand, Chris Ramsey, Michael Johnson, Ricky Hill, Paul Davis na Sol Campbell wamejiunga na wito wa Corinaldi kutaka malengo ya ushirikishwaji na ujumuishwaji wa watu wa jamii mbalimbali yawemo katika Mswada wa Utawala wa Soka.

Pia wametoa wito kwa wadau wa soka kufanya kazi na BFP ili kuelewa ubaguzi katika mchezo huo na kwa wanasoka weusi kupata msaada wanaohitaji ili kujiendeleza kila ngazi ya mchezo bila kuzuiwa na chuki au ubaguzi wa rangi.

'Mdhibiti huru anaweza kutoa fursa lakini ikiwa hatashughulikia usawa wa rangi katika mchezo kulingana na data zinavyoonyesha basi itakuwa ni fursa iliyokwenda bure. Ripoti hii ni fursa kwa mchezo wa soka kujiunda upya, kushirikiana tena na BFP ili tufanye kazi kuelekea suluhisho endelevu," aliongeza Corinaldi.

# Ras Nganyagwa katika mabonde na milima ya muziki

## ● Anasimulia mwenyewe mikasa hadi mafanikio ya sasa

***Mwanamuziki mkongwe wa muziki wa Raggae, Innocenti Nganyagwa ameamua kusimulia safari yake ndefu ya kimuziki kama inavyoletwa hapa na gazeti lako hili la Uelekeo. Tupate uhondo huo katika sehemu hii ya kwanza ya simulizi yake.***

MWISHONI mwa miaka ya 80 kuelekea mwanzoni mwa miaka ya 90 kulikuwa na Bendi inaitwa MCA Orchestra ilikuwa na Makao yake Makuu Mabibo hapa jijini.

Bendi hiyo ilitumia Mtindo wake wa 'Munisandesa' (Muziki ni Safari Ndefu Sana) niliipenda bendi hiyo si tu kwa ajili ya uwezo wake kimuziki na wanamuziki wake mahiri, lakini pia ukweli wa maana ya jina la mtindo wao walilolibuni.

Nimepitia 'Mtindo' huo kwenye 'msoto' wangu kimuziki, hapo pichani juu ni zama ambazo nilikuwa sijafanikiwa kuingia kurekodi studioni kurekodi, lakini nilikuwa na usongo kupitiliza, niliasisi bendi nikiwa Iringa tukajirekodi mazoezini, nikajitengenezea Kava nikajiandika jina langu na la bendi na albamu!

Dhamira njema siku zote hutimiza ndoto maishani hatimaye 'nikatoboa' kupitia albamu ya 'Life Controversies' ambayo baadaye ikatoka kwa jina la 'Money Pesa' mwaka 1994 ikiwa na wimbo wa Gila ambao mashabiki huuita 'Wimbo wa Taifa wa Reggae'.

Huyooo....Mdogo Mdogo:

Kama walivyoimba Orchestra MCA kwamba muziki ni safari ndefu sana (MUNISANDESA), ndiyo yalivyo maisha yangu katika muziki. Nilitunga wimbo wangu wa kwanza nikiwa darasa la nne, baadaye nikawa mcheza disko 'Disco Dancer' , halafu Dj huku nikiendelea kutunga tungo nyingi zaidi ndipo baadaye nikageukia rasmi Mipini. Hiyo ilikuwa kule kitongojini Keko Juu Kata ya Miburani, Manispaa ya Temeke, nikamfahamu Richard Ndunguru Mwalimu wangu wa Muziki aliyeunda bendi ya The Wailing Peasants mwaka 1989 nami nikawa mpiga drums mwandamizi na baadaye kujifunza magitaa ya besi na Rhythm.

Bendi iliposhindwa kuendelea kwa sababu za kiuchumi nikaenda Iringa kwa Baba Mzazi huko nikajiunga na Bendi ya Vijana Consolata Orchestra (VICO) iliyomilikiwa na Kanisa Katoliki Parokia ya Consolata kitongoji cha Mshindo, Iringa Mjini.



# Vinicius aongoza kwa kubaguliwa Hispania

**MADRID, Hispania**

BRAZIL walikuwa wametoka kuifunga England 1-0 mwezi uliopita wakati wanahabari walipomwendea Vinicius Jr kwa mahojiano katika eneo la mchanganyiko la Wembley.

"Lakini tutazungumza juu ya mpira wa miguu?" fowadi wa Real Madrid alijibu kwa tabasamu.

Baada ya jibu hilo, alikubali kujibu maswali machache. Baada ya kugundua kuwa atafanya mkutano na waandishi wa habari huko Madrid siku chache baadaye ambapo ungetawaliwa zaidi na vita vyake vya kibinafsi dhidi ya ubaguzi wa rangi, Vinicius alitaka kukwepa mada hiyo huko London.

Na ndivyo alivyofanya. Lakini basi, alipokuwa akizungumza kabla ya mechi ya kirafiki ya Brazil dhidi ya Uhispania, aliangua kilio alipokuwa akizungumzia madhara ya unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi anayoendelea kuyapata katika viwanja vya Uhispania.

"Nataka tu kucheza kandanda, lakini ni vigumu kusonga mbele. Najisikia huzuni na huzuni zaidi na hamu ya kucheza inapungua," alisema na kuongeza; "Nikiwa na umri wa miaka 23, lazima niwafundishe Wahispania wengi kuhusu ubaguzi wa rangi."

Kwamba supastaa wa klabu kubwa na timu ya taifa duniani alikuwa amefikia hatua ya hata kufikiria mustakabali wake katika hatua hii ya maisha yake ya soka ilidhihirisha tu jinsi hali ilivyo.

La Liga ilirejelea matukio 10 ya ubaguzi wa rangi yanayomhusisha Vinicius kwa waendesha mashtaka wa Uhispania msimu uliopita, lakini inaonekana ni machache sana yaliyoshughulikiwa hadi sasa.

Wakati Real Madrid watakapomenyana na Manchester City siku ya Jumanne katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, huenda namba saba asiwee kama mchezaji mwenye kipaji zaidi kwenye uwanja wa Santiago Bernabeu ingawa ni miongoni mwa wanaoangaziwa.

Lakini pengine ndiye mwanasoka muhimu zaidi duniani kwa sasa.

Pambano lake linakwenda zaidi ya soka.

Katika miaka ya hivi karibuni, Vinicius amekuwa sauti nyeusi inayoongoza katika kukabiliana na changamoto za ubaguzi wa rangi katika soka na, licha ya mzigo wa kihisia iliomletea, hana nia ya kurudi nyuma.

"Vinicius anavunja ukimya uliokuwa ukizunguka suala hili na uliwekwa na tasnia ya kandanda siku za nyuma," Marcelo Carvalho, mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Observatory of Racial Discrimination in Football, aliiambia Shirika la Haabari la BBC.

''Anapigana na mfumo ambao umesheheni ubaguzi wa rangi"

Hata hivyo, hakuna hata moja kati ya hayo ambayo yalimtayarisha kwa kile atakachokabiliana nacho Hispania baada ya kuondoka Flamengo na kujiunga na Real Madrid akiwa na umri wa miaka 18 mwaka 2018, huku kukiwa na matusi mengi kutoka kwa stendi, nyimbo za nyani na sanamu iliyotundikwa kwenye daraja.




"Nimeangalia nyuma kidogo na sijawahi kuona mchezaji ambaye amenyanyaswa kama Vinicius," mkufunzi wa Real Madrid Carlo Ancelotti alisema mwezi uliopita.

Huo ndio ukali wa hali ambayo imegeuka kuwa suala la kidiplomasia, huku serikali ya Brazil ikimwita balozi wa Uhispania kuelezea matukio hayo na kutaka hatua za kukomesha.

Wakati hisia ya kutokujali inabaki, Vinicius anafanya kazi peke yake.

Mwaka jana, fowadi huyo alizindua kampeni chini ya kauli mbiu "Ubaguzi wa rangi, usijifanye hauoni" kwenye mabango kote nchini mwake na hata nje ya nchi kwa Siku ya Uhamasishaji Weusi.

Pia amesaidia kukarabati shule kadhaa nyumbani kupitia taasisi yake na kutoa mwongozo wa kupinga ubaguzi wa rangi ili kufanya mazingira ya elimu kuwa shirikishi zaidi.

Amekuwa akiongea kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kesi za ubaguzi wa rangi zinazohusisha wanasoka wengine pia.

"Mipango hii ni yake kwa 100%. Tunachofanya ni [kuifanya] na kumpa nguvu zaidi ya kupigana. Tunatoa ushauri, lakini mwisho ni mapambano yake. Hakuanzisha vita dhidi ya ubaguzi wa rangi kutoka kwa papo hapo. Aliteseka," akaeleza wakala wake Frederico Pena. "Yeye ni mpiganaji. Yeye daima imekuwa. Inaendesha katika familia."



**Nataka tu kucheza kandanda, lakini ni vigumu kusonga mbele. Najisikia huzuni na huzuni zaidi na hamu ya kucheza inapungua," alisema na kuongeza; "Nikiwa na umri wa miaka 23, lazima niwafundishe Wahispania wengi kuhusu ubaguzi wa rangi"**

# Wasanii mnafuatilia haki zenu COSOTA?

## ● Ama ziliondoka na Mzee wa ‘Ukweli na Uwazi’ Mkapa!
## ● ‘Bongo Movie’ badilikeni ili kuwinda soko la Afrika

**Na Hamid Yassin**

SIKUSUDII kuamsha upya hisia za huzuni zilizogubika taifa Julai 24, 2020 mara tu baada ya kusikia taarifa ya hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli akitangazia umma juu ya kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Benjamin William Mkapa.

Ni dhahiri kuwa kifo cha Rais huyo mstaafu na mwanadiplomasia mkongwe kilikuwa ni pigo kwa taifa, Afrika pamoja na dunia kufuatia mchango wake ulioakisi mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, mahusiano ya kimataifa na mapinduzi katika sekta za umma na binafsi nchini.

Hakika, Watanzania hawana budi kujifunza mambo mengi aliyoyafanya Mzee Mkapa na pia kumuenzi kwa kuthamini mchango wake uliosaidia kuleta mabadiliko katika kuleta maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Katika uongozi wake Mzee Mkapa alianzisha mikakati ya kimaendeleo kwa jamii katika nyanja mbalimbali. Achilia mbali ya kutuachia Uwanja mkubwa wa Taifa ambao sasa upo kwa jina lake la ‘Mkapa’, lakini nyanja nyingine ambazo chini ya uongozi wake ziliandaliwa kimkakati ni uendelezaji wa sanaa na muziki.



Hayati Benjamin William Mkapa

Kama tunavyokumbuka, sekta ya sanaa na muziki kwa miaka mingi ilikuwa na changamoto nyingi husussan kuwepo kwa dhuluma kwa wasanii na wanamuziki ambao wamekuwa wakitegemea kazi zao kwa lengo la kujipatia kipato.

Wamekuwa wakitengeneza filamu na kutunga nyimbo ambazo hazikuwanufaisha wasanii kutokana na kudhulumiwa, sababu kubwa ilikuwa ni kukosekana kwa Sheria ya Hakimiliki enzi hizo.

Kufuatia kilio cha muda mrefu cha wasanii kuibiwa kwa kazi zao, Mzee Mkapa alianzisha Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA), chombo ambacho ni cha kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 46 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya mwaka 1999.

Chombo hiki kilipewa mamlaka ya kusimamia Sheria ya Hakimiliki.

Hatua hii ilikuwa ni mwanzo wa safari ndefu ya wasanii na wanamuziki katika kuwaletea mafanikio makubwa ikilinganishwa na sheria ya zamani ambayo miongoni mwa mambo mengine, haikuweka kipengele cha kusimamia Hakimiliki za wasanii na wanamuziki.

Licha ya kusimamia Hakimiliki, kazi nyingine za COSOTA ni kukuza na kulinda maslahi ya waandishi wa vitabu, waigizaji, wafasiri, wachapishaji, watengenezaji wa rekodi za santuri, watangazaji na wachapishaji na hasa kukusanya na kusambaza mirabaha yoyote na malipo mengine yanayostahili kuhusiana na haki zao.

Aidha, chama hiki pia ni kiungo kati ya wamiliki wa haki kwa upande mmoja na watumiaji wa kazi zao kwa upande mwingine.

Ni dhahiri shahiri kuwa Mzee Mkapa alizingatia maslahi mapana ya watu wanaojihusisha na kazi za sanaa, uandishi na utangazaji na hivyo kutokana na kifo chake kile Watanzania tuna kila sababu ya kuendeleza kila zuri alilolifanya.

Sambamba na kujifunza namna bora ya kuendeleza vipaji, kazi za sanaa na kila mmoja kuchangia kwa namna yake kwa lengo la kuboresha maisha katika jamii, kupunguza umasikini kama yalivyokuwa maono yake kwa taifa hili.

Katika kitabu alichoandika Mzee Mkapa miezi kadhaa kabla ya kifo chake na kuzinduliwa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati Dk. John Pombe Magufuli, alielezea juu ya maisha yake binafsi.

Katika kitabu hicho chenye jina la “Maisha Yangu, Dhamira Yangu:

Rais wa Tanzania Akumbuka,” Mzee Mkapa pamoja na kugusia masuala mengi, lakini pia alielezea juu ya maono yake; “ ni maisha ya hali ya juu, amani, utulivu na umoja, utawala bora, jamii iliyoelimika na uchumi shindani wenye uwezo wa kukua kiendelevu na mgawanyo shirikishi wa kipato!”

Sasa basi funzo la kifo cha Mzee Mkapa kwa wasanii kwa ujumla wakiwemo wa filamu, maarufu kama ‘Bongo movie’ ni lipi? Ama upi mchango wa Bongo movie kwa taifa?

Mbali na mafunzo yaliyopatikana katika filamu zile za awali za Nsuka, dereva Tax na ile ya Chausiku, ambayo siwezi kusahau kwani ina radha yake ya maisha ya uswazi, au ile ya kitambo ya ushuani ya Girlfriend iliyotoka mwaka 2003 ikiwa ni filamu iliyoleta mapinduzi katika sekta ya uigizaji nchini.

Nadhani wakati umefika sasa watengenezaji wa filamu na wadau wote wa tasnia hiyo wakaanza kuandaa filamu zenye maslahi mapana ya taifa, kuhusu masuala mbalimbali mfano historia ya nchi, maisha ya viongozi mbalimbali kama vile Mama Getrude Mongella namna alivyowakilisha nchi katika Mkutano wa Beijing mwaka 1990, ukombozi wa bara la Afrika na mambo kadha wa kadha.

Hapo Bondeni (Afrika ya Kusini) waliandaa filamu kuhusu maisha ya baba wa taifa lao Mzee Nelson Mandela, Marekani wao na filamu zao kama za Barrack Obama, Ton Braxton, Black Panther na ile ya The White house.

Nafahamu kuwa wametuzidi kwa teknolojia na taaluma kuhusu uandaaji wa filamu lakini bado naamini hata sisi tuna ubunifu na tunaweza kuandaa filamu zetu kwa teknolojia yetu, mazingira yetu na ubunifu wetu.

Ndugu zangu wa Bongo movie, baada ya kusoma makala hii pengine mtataharuki mkidhani nimewachana kwa ubaya, la hasha! Hakika dhamira yangu ni kuona filamu zetu zinakuwa zaidi ya kuonesha mapenzi na hadithi za kawaida sana. Hakuna ubaya hata kidogo mki-act kuhusu historia ya nchi yetu.

Nchi imepitia matukio mbalimbali, lakini katika filamu zetu kwa kiasi kikubwa maudhui ni yale yale tena utakuta mwanamke wa kijijini eti amevaa wigi, kucha ndefu mithili ya chui, rangi ya mdomo imekolea utadhani ametoka kuchinja kuku kwa mdomo!

Kijana wa kiume mwenye mkorogo, hereni masikioni achilia mbali tattoo zilizomjaa mikononi na miguuni. Kuhusu lugha, hapa nako kuna vioja vyake kedekede. Si ajabu wengi wenu mmewahi kuangalia filamu ya Kiswahili lakini jina (tittle) lake limeandikwa kwa lugha ya Kingereza. Hebu tujiulize, ni nani amewahi kuangalia filamu ya kihindi yenye jina (title) lililoandikwa Kihispania? Mmeona wapi? Kuhama kwa COSOTA kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara kwenda Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutaakisi mabadiliko yanayohitajika kulingana na wakati uliopo. Ni wazi kuwa Watanzania wakiwemo wasanii bado wanamkumbuka Mzee Mkapa kutokana na jinsi alivyowaondoa katika unyanyasaji, na dhuluma kwa kuibiwa kwa kazi nyingi walizokuwa wakizifanya kwa jasho lao.

Leo hii Watanzania, hususan wasanii wa Bongo movie jiulizeni ni kitu gani cha msingi zaidi ambacho mnakifanya katika kumuenzi Mzee Mkapa? Ni wazi kuwa aliwajali na kuanzisha COSOTA ili iwasaidie kulinda kazi zenu sambamba na kuongeza thamani ya vipaji mlivyonavyo ili muweze kupata fedha zitakazowasaidia nyinyi na familia zenu.

Wenzenu wasanii wa muziki hususani Bongo Fleva wanafaidika sana na mirabaha ya kazi zao; Je, nyie pia mnafanya hivyo au mpaka COSOTA iwafuate majumbani kwenu? Waluguru wana msemo wao usemao ‘Kalaghabao’!

> “ **Kufuatia kilio cha muda mrefu cha wasanii kuibiwa kwa kazi zao, Mzee Mkapa alianzisha Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA), chombo ambacho ni cha kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 46 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya mwaka 1999.**



Wasanii wa Bongo Movie

## Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa
Simu: +255 765 828 219

# Mtoko wa Eid







EID ni nini? Wakati wa Sherehe na Mavazi ya Kifahari!

Eid al-Adha au Sikukuu ya Sadaka ni tukio la furaha linaloadhimishwa na Waislamu kote ulimwenguni. Tamaduni inayopendwa sana wakati wa sikukuu ya Eid ni kuvaa mavazi mazuri ya mtu ili kushiriki katika sala maalum na furaha. Kwa kushikilia heshima na heshima, mara nyingi wanawake huchagua mavazi ya kitamaduni ya Kiislamu, kama vile abaya, kaftan na nguo za maxi, wakati huu.

Unapojitayarisha kwa ajili ya sherehe, ni muhimu kuchagua mavazi mazuri ya Eid. Hii ni fursa ya kuonyesha mtindo wako wa kipekee huku ukihifadhi msingi wa mavazi ya kawaida ya wanawake. Pamoja na wingi wa chaguzi, kazi ya kuchagua mkusanyiko bora wa Eid inaweza kuonekana kuwa nzito.

Katika mwongozo huu unaojumuisha yote, tutakusaidia katika kugundua mitindo ya Eid, kukupa ushauri na mapendekezo muhimu ya mavazi yanayovutia ambayo yanahakikisha unasherehekea kwa ujasiri!

Tokelezea na nguo ya stara kama abaya

### ABAYA

Abaya zimekuwa vazi la Kiislamu lisilopitwa na wakati ambalo mara kwa mara linajumuisha staha kwa wanawake. Vazi hili linalotiririka na tulivu hufunika mwili mzima, na kuifanya kuwa chaguo bora kwa sikukuu ya Eid. Abaya zinapatikana katika mitindo na mifumo mingi, ikizingatia mapendeleo yote. Chagua kutoka kwa chic, abaya nyeusi iliyosafishwa au chunguza miundo tata iliyopambwa kwa embroidery, lace au sequins. Kamilisha abaya yako kwa hijabu inayolingana na vifaa vya kifahari ili kupata mwonekano maridadi na mashuhuri wa Eid.

Vifaa mbalimbali vya Eid ambavyo vitainua mwonekano wako na kukufanya ujiamini na kuwa maridadi katika msimu huu wa sikukuu.

### VITO VYA TAARIFA


Hakuna vazi la Eid ambalo limekamilika bila vito vya kupendeza. Chagua vipande vya kauli kama vile pete kubwa, mikufu iliyotiwa safu, au vikuku vidogo ili kuongeza mguso wa kuvutia kwenye vazi lako. Zingatia miundo ya kitamaduni kama vile jhumkas, maang tikka, au choker zilizopambwa kwa vito vya rangi ili kukidhi mavazi yako na kukumbatia mila za kitamaduni.

### MIKOBA NA CLUTCHES

Vinaweza kuinua mkusanyiko wako wa Eid papo hapo huku ukiweka mambo yako muhimu karibu. Tafuta mikoba iliyopambwa kwa ustadi au mikoba iliyopambwa inayolingana au inayosaidia vazi lako. Mitindo ya metali, maelezo ya shanga, au mifumo iliyopambwa inaweza kuongeza kipengele cha ziada cha uzuri na kisasa kwa mwonekano wako wa jumla.







Kwa wale wanaovaa hijabu au mitandio, Eid ni wakati mwafaka wa kuonyesha mtindo wako wa kibinafsi. Chagua kutoka kwa anuwai ya vitambaa, rangi, na mifumo inayosaidia mavazi yako. Zingatia mitandio ya hariri iliyo na chapa tata, hijabu za chiffon nyepesi na za kudarizi maridadi, au vifuniko vya kifahari vya satin ili kuongeza mguso wa umaridadi kwenye mwonekano wako.

Viatu vyako vina jukumu muhimu katika kukamilisha mkusanyiko wako wa Eid. Chagua chaguzi maridadi na za starehe zinazolingana na mavazi yako. Mojris iliyopambwa ya kitamaduni au viatu vilivyopambwa vinaweza kuongeza mguso wa kitamaduni, wakati visigino vilivyo na laini au gorofa katika vivuli vya metali vinaweza kuipa mavazi yako makali ya kisasa. Chagua viatu ambavyo sio tu vinalingana na mavazi yako lakini pia hukuruhusu kusonga kwa raha na kufurahiya sikukuu.

### SAA NA BANGILI

Saa na bangili ni vifaa vingi vinavyoweza kuinua vazi lako la Eid bila shida. Chagua faini za metali kama vile dhahabu, fedha au waridi, na uchague miundo inayoendana na mtindo wako wa kibinafsi. Bangili maridadi au saa ya kauli inaweza kuongeza mguso wa hali ya juu na kukamilisha mwonekano wako kwa ujumla.

### HENNA

Kupaka hina, hasa kwa sherehe kama Eid, ni utamaduni wa jumuiya. Wanawake wa rika zote huja pamoja ili kupaka hina kwa kila mmoja, kuunda na kuthibitisha hisia ya udada na jumuiya. hina huendana na mapambo kama saa,bangili pete na kucha,ili urembo wa mikono ukamilike hina ni maridhawa kuwepo.

Eid ni tukio maalum ambalo linahitaji mtindo mzuri kutoka kichwa hadi vidole. Kwa kujumuisha vifaa vinavyofaa kwenye vazi lako, unaweza kuongeza mguso wa kibinafsi na kuunda mkusanyiko mzuri unaoakisi mtindo wako na mila za kitamaduni. Iwe ni vito vya taarifa, mikoba maridadi, mitandio ya kifahari, au vifaa vingine, miguso hii ya kumalizia itaboresha mwonekano wako wa Eid na kukufanya ujiamini na maridadi katika sikukuu zote. Kubali ari ya furaha ya Eid kwa kujipamba kwa vifaa hivi bora kabisa.



Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Aprili 10 - 16, 2024 |


# Simba yang'olewa CRDB FA

**Mwandishi Wetu**

KWA mara nyingine timu ya Mashujaa ya Kigoma imeing'oa Simba kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho la CRDB baada ya kufanya hivyo mwaka 2018.

Mashujaa ambao mwaka 2018 walishinda ndani ya dakika tisini bao 3-2, safari hii wamefanikiwa kutinga robo fainali kwa njia ya matuta kwa kufunga penalti sita kati ya saba walizopiga huku Simba ikiambulia penalti tano kati ya saba walizopiga.

Shujaa wa Mashujaa ni nahodha wao Baraka Mtui aliyefunga penalti ya mwisho kati ya zile za nyongeza huku Sadio Kanoute akikosa tuta la mwisho kwa upande wa Simba.



# Simba yatamba kulipa kisasi Aprili 20






**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba imesikia majigambo ya watani wao Yanga kwamba Aprili 20 watawapa dozi kubwa zaidi ya ile ya Novemba 5 mwaka jana lakini imewataka wasahau hilo kwani wamejipanga kulipa kisasi cha kishindo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally ameliambia Uelekeo kwamba amemsikia mwenzake Afisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe akijinasibu watawafunga tena hapo Aprili 20, lakini amejibu mapigo kuwa hilo haliwezekani na kusisitiza watani wao hao hawataamini kitachowakuta siku hiyo.

Akiongea kwa njia simu toka Kigoma walipokwenda kucheza mechi ya Kombe la Shirikisho la CRDB dhidi ya Mashaujaa jana, Ahmed amesema Simba inajua wapi walipofanya makosa mpaka wakabugizwa bao 5-1 katika mechi ile ya Mzunguko wa kwanza na kamwe hawatarudia makosa.

"Kocha wetu wa sasa Abdelhak Benchikha hakuwepo kwenye lile pambano la awali, lakini baada ya kumpatia mikanda ya video na kuiangalia ile mechi kwa makini ametuhakikishia Yanga inafungika bila shaka yoyote," amedai Ahmed.

Meneja huyo wa Habari wa Simba ambaye wiki yote hii amekuwa akiwacharura watani wao hao kufuatia kulalamikia goli lao lililofungwa na Aziz Ki dhidi ya Mamelod na kukataliwa na refa mwenye beji ya FIFA kutoka Mauritania, Beida Dahane, ametamba kwamba mbali ya Benchikha kuwapa matumaini hata wao viongozi wanajua walipojikwaa na Yanga kutumia fursa ile kuwaadhibu.

Akizungumzia maandalizi ya pambano hilo la kisasi na kukata na shoka, Ahmed amesema hakutakuwa na maandalizi maalumu kutokana na kubanwa na ratiba ya mechi mfululizo za Ligi Kuu ya NBC, hata hivyo wanajua watafanya nini wiki moja kuelekea mechi hiyo na mahasimu wao.

Mara baada ya Bodi ya Ligi kutangaza tarehe ya mechi hiyo kufuatia wakongwe hao wa soka la nchi hii wote kutupwa nje ya Ligi ya Mbaingwa Afrika, Kamwe aliwataka Simba wajiandae kisaikolojia kwani Aprili 20 watawapiga kipigo kitakatifu kuliko kile cha Novemba 5 mwaka jana.

# TOT yashusha vibao vipya kumuenzi Dk. Samia

## ●Kuipuliwa kwenye Tamasha kubwa Aprili 20




**Na Mwandishi Wetu**

KUNDI la Sanaa la Tanzania One Theatre (TOT), limeipua vibao kadhaa maalumu vya kuenzi kazi zilizotukuka zilizofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika miaka yake mitatu.

Hayo yamewekwa hadharani na Katibu Mipango wa TOT, Omari Mussa Jenela al maarufu kama Bokilo na kuongeza kuwa, uzinduzi wa nyimbo hizo utafanyika kwenye Tamasha maalumu kubwa litakalofanyika Aprili 20 kwenye viwanja vya TTCL Kijitonyama.

Bokilo amezitaja nyimbo hizo kuwa ni pamoja na 'Jicho la Mama' na 'Dk. Samia Mwamba' ambazo ni za dansi huku upande wa kwaya wanakuja na nyimbo za 'Kanyaga twende' na 'Twende kwa pamoja' zilizotungwa na mwimbaji wa kundi hilo, Meka Twalib huku kibao cha tatu kinachokwenda kwa jina la 'Kazi iendelee' kimetungwa na msanii mwingine wa kundi hilo, Peter Kakondeli.



Katibu Mipango huyo ambaye pia ni kiongozi wa shoo wa TOT, amepasha kuwa, kutakuwa na wimbo maalumu wa Chama uliotungwa na Omari Ally, lakini wanahifadhi jina lake hili kuwashtukiza mashabiki nwao.

Mbali na nyimbo hizo za dansi na kwaya za kumuenzi Dk. Samia, pia Bokilo amesema kutakuwa na burudani ya nyimbo za mipasho, yaani taarab ambapo watakaohudhuhuria Tamasha hilo, watapata fursa ya kusikia vibao vipya vinne maridhawa sambamba na nyimbo zote za zamani za dansi, kwaya na taarab za kundi hilo.

"Hatutawaacha hivi hivi, tutawapigia hadi nyimbo zetu za zamani kama vile 'Mtaji wa Maskini,', 'Aminata', 'Mtu Pesa', 'Walimwengu', 'Kisa cha Mpemba', 'Jirani' na nyingine kadhaa," amesema Bokilo.